

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Saba – Tarehe 5 Novemba, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge atakayeuliza swali la kwanza kwa leo kwa kuwa leo ni siku ya historia kwa Afrika na kwa duniani ya watu wenye asili ya Afrika napenda kwa niaba yenu nitangulize pongezi nzito sana za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Rais Mteule wa Marekani, Rais Barack Obama, kwa ushindi wake mkubwa sana usio hata na mashaka ambao ametupatia.

Waheshimiwa Wabunge, ni heshima kubwa sana kwa Afrika, heshima kubwa sana kwa Afrika Mashariki, kwa sababu anatoka nchi ya jirani.

Nimetaarifiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwamba anaandaa nakala ya azimio la Bunge nadhani tutalipata kabla hatujamaliza shughuli ya asubuhi ili tuweze kulipitisha rasmi na likae katika historia ya nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 84

**Utekelezaji wa Ahadi Zilizotolewa wakati wa
Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005**

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa ahadi mbalimbali kama vile uboreshaji wa Miundombinu hususan barabara na umeme pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania:

- (a) Je, Serikali itatumia njia gani kutekeleza ahadi zote zilizotolewa?
- (b) Je, kipimo cha kumpatia kila Mtanzania maisha bora kikoje hadi kufikia mwezi Aprili, 2008?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niongeze sauti yangu ya kumpa pongezi za dhati kabisa Rais Mteule wa America Barack Hussein Obama nasikia Shangwe haziko tu Kisumu na hata RoRya. Hapa Bungeni akina Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Sarungi, Massaburi nasikia wanasherehekea. Huyu ni Rais wa 44 wa nchi kubwa ya America.

Hii ni ishara kwamba ndoto ya wana harakati akina *Martin Luther King Junior* baada ya miaka 50 sasa imetimia na sote tuwapongeze sana wananchi wa *America* kwamba katika nchi ile kubwa kila kitu kinawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa ahadi mbalimbali kama vile uboreshaji wa miundombinu hususan barabara na umeme pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Katika kuhakikisha ahadi hizo zinatekelezwa kikamilifu Serikali itumia Bajeti yake na kuwashirikisha wananchi na wafadhili mbalimbali katika miradi ya huduma za jamii kama vile elimu na afya na huduma za kiuchumi kama vile ujenzi wa barabara na umeme. Aidha, ni azma ya Serikali kuongeza Bajeti ya sekta ya miundombinu kila mwaka kadri hali ya fedha, inavyoruhusu na kuhamasisha umuhimu zaidi kuwahimiza makandarasi wazalendo kujengo ushirikiano na wawekezaji wakubwa kutoka nje kwa lengo la kujenga uwezo wa makampuni ya ndani na kuongeza mitaji katika ujenzi wa miundombinu yetu.

Kwa upande wa umeme, sheria mpya iliyotungwa katika Bunge hili Tukufu Aprili, 2008 ya kutoa ushindani kwa *TANESCO* kutaongeza huduma ya umeme kwa wananchi na hivyo kuwawezesha kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Katika kuboresha huduma za umeme vijijini, wakala wa Nishati vijijini ilipata shilingi bilioni 10 katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 kutekeleza mpango wa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya kama vile Kilolo, Orkesumet, Kilindi, Mkinga, Uyui na Bahi. Mwaka huu 2008/2009 Serikali imetenga shilingi bilioni 20 zitakazotumika kusambaza, kuhifadhi na kufikisha huduma ya umeme vijijini.

(b)Mheshimiwa Spika, vipimo vya maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na ongezeko la kipato na upatikanaji wa huduma za msingi za maji, elimu, afya, umeme, barabara na kadhalika. kwa ujumla pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka shs. 361,309 mwaka 2002 hadi shilingi 548,388 mwaka 2007, huduma za msingi zimeboreshwa na kuwafikia Watanzania wengi zaidi.

Uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi na wanaojiunga na sekondari umeongezeka maradufu. Vile vile idadi ya shule za msingi imeongezeka kutoka 14,700 mwaka 2006 hadi 15,624 mwaka 2007.

Hivi sasa tuna vyuo vikuu 32 na kati ya hivyo 11 ni vyuo vya Serikali na 21 ni vyuo vya binafsi. Wanafunzi waliosajiliwa katika taasisi hizo iliongezeka kutoka 35,606 mwaka 2006 hadi 64,878 mwaka 2007 sawa na ongezeko la asilimia 82.2. Maji, barabara na sekta zote za umwagiliaji maji mashamba, visima vya maji kwa ajili ya mifugo vile virefu na vifupi vimechimbwa na vingine kukarabatiwa ili kutoa huduma karibu na walengwa.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali kuwawezesha wananchi kuongeza na kuboresha upatikanaji wa huduma bora ili kumpatia kila Mtanzania maisha bora iko pale pale na inaendelea.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kina ukipenda naomba kuongeza swali moja.

Miongoni wa ahadi za Serikali ni ajira milioni 1 katika nchi yetu. Je, ajira zimefikia wapi hadi leo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, nimetoa takwimu na hii ni ishara kwamba majibu haya siyo Sadick ukipenda lakini Mheshimiwa Mbunge anaweza akawa na maoni yake ana uhuru wa kuwa na maoni hayo. Ajira, milioni 1 ni mchakato kati ya 2005/2010 takwimu za sasa zinaonyesha tumepita zaidi ya nusu kupata ajira hizo milioni 1. Kwa hiyo, tunalihakikishia Bunge hili na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itahakikisha kuwa ajira milioni 1 itafikiwa kabla ya mwaka wa 2010. *(Makofi)*

MHE. KHALIFA S. KHALIFA: Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida mwananchi anaona nafuu maisha kama anatimiza milo yake mitatu ya kila siku. Kwa hali halisi tuliyo kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa mara kwa mara hasa za vyakula na mafuta na mambo mengine ambapo Serikali haionekani kuwa makini katika kusimamia

bei za bidhaa hizi hali ya wananchi ni mbaya kwa sababu wengine hata hiyo milo hawatimizi. Je, Waziri anasemaje juu ya hili? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hali ya uchumi ya mtu mmoja mmoja siyo nzuri sana. Lakini kama nilivyosema maendeleo ya uchumi ni mchakato lakini pia tukumbuke hali ya sasa ya dunia siyo nzuri hata kidogo. Bei ya mafuta imepanda na sisi hatuna mafuta, bei ya chakula imepanda lakini kwa jitihada za Serikali yetu mfumko wa bei katika nchi yetu ni mdogo sana ukilingalisha na nchi zinazotuzunguka sasa.

Hali hii ya mfumko wa bei kuwa chini ni ishara kwamba kuna jitihada za kipekee za hali ya juu kabisa za Kiserikali kuhakikisha kwamba angalau mwananchi wa kawaida anapata ahueni.

Na. 85

Vita Dhidi ya Madawa ya Kulevya

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. STEPHEN JONES GALINOMA) aliuliza:-

Kwa kuwa Kisheria ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kushughulikia makosa yote ya uhalifu wa jinai ikiwa ni pamoja na dawa za kulevya;

- (a) Je, ni kwa nini kuna kitengo katika Ofisi ya Waziri Mkuu kinachoshughulikia suala hilo hilo?
- (b) Je, kina tofauti gani ya ziada kwa kitengo hicho na Wizara husika na Serikali haioni kuwa huko ni sawa nakutawanya nguvu zake?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma (Kalenga) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Tatizo la dawa za kulevya nchini na duniani kote siyo tu suala la kijinai (*crime issue*) bali ni tatizo linalogusa sekta nyingi (*multi-sectoral*) mfano ya kijamii, kiafya, kiuchumi, kisiasa na kadhalika. Pia linaingia kwenye uhalifuwa kimataifa. Baada ya kuleta madhara mengi yaliyotokana na dhana iliyokuwepo awali ya kulichukulia tatizo ladawa za kulevya kuwa la kijinai pekee likishughulikiwa na vyombo vya dola tu, dunia iligundua kwamba mbinu mbadala shirikishi za kukabiliana na janga hili zinajihitajika. Mbinu hizo zimepelekea kuanzishwa kwa mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa za

kupambana na biashara hiyo haramu. Mikataba na itifaki hizo zinazitaka nchi wanachama kuwa na vyombo maalumu vya kukabiliana na tatizo hili kwa wigo mpana zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya mikataba ya kimataifa Serikali iliamua kutunga sheria namba 9 ya mwaka 1995 iliyounda Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya Nchini inayoongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Tume hiyo inayo majukumu mapana sana yale ya Kitengo cha Dawa za Kulevya chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pia zimeongezewa nguvu.

Tume inafanya kazi ya uratibu na kuviunganisha na kuvishirikisha Vyombo vya Dola kudhibiti na Kupambana na tatizo la dawa za kulevya ili kuleta ufanisi. Baadhi ya vyombo hivyo ni Polisi, Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya, (ADU), Idara ya Ushuru wa Forodha, Idara ya Uhamiaji, Posta, Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Asasi za Kijamii, na kadhalika.

(b)Mheshimiwa Spika, Kitengo chini ya Jeshi la Polisi kinapeleleza, kinachunguza na kukamata dawa za kulevya, mali na watuhumiwa ili hatimaye kuwafungulia mashtaka. Kazi kubwa ya Tume ni kusimamia Sheria, kuainisha, kutangaza na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na kutoa elimu na kukuza ushirikiano na wadau wa ndani na wa nje ya nchi.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi, kwamba vyombo hivyo viwili havifanyi kazi moja ila vinashirikiana kiutendaji na mgawanyo wake wa majukumu uko wazi kabisa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakati tunachambua Bajeti mwezi Mei Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliishauri Serikali kuongeza Bajeti ili kitengo hiki cha kupambana na madawa ya kulevya waweze kufanya majukumu yao vizuri. Je, Mheshimiwa Waziri ana maelezo gani kuhusu kukiongezea Bajeti kitengo hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati tukichambua wakati bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kamati ilipendekeza bajeti ya Tume ya kudhibiti dawa za kulevya iongezwe nakumbuka tuliahidi kwamba kadri hali ya uchumi itakavyokuwa nzuri tutaongeza bajeti ya tume hii.

Lakini pia ikumbukwe nilielezea kwamba kwa kuona hili Serikali imeanzisha mchakato wa kupandisha hadhi tume hii ili iwe mamlaka hii yenye kasma yake na itakuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Waraka wa Baraza la Mawaziri umeandaliwa ili hatimaye sheria ya kuunda mamlaka kamili ya dawa za kulevya iweze kuletwa Bungeni.

Kutengeneza Barabara ya Mawenzi – Kisukuru kwa Kiwango cha Lami

MHE. MGANA I. MSINDAI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kutengeneza barabara ya Tabata toka Bima, Mawenzi – Kisukuru kwa kiwango cha lami lakini mpaka sasa lami imeishia Mawenzi:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo toka Mawenzi mpaka Kisukuru kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tabata kuanzia Bima kupitia Mawenzi hadi Kisukuru ina urefu wa kilomita 4.8. Barabara hii ni kiungo muhimu na inahudumia wananchi wa maeneo ya Tabata, Kisukuru, Segerea, Kinyerezi, Mawenzi na inaunganisha Manispaa ya Kinondoni na Ilala.

Vile vile barabara hii hutumika kusaidia kupunguza msongamano wa magari Jijini hivyo kufanya umuhimu wake kuwa na hali ya juu. Manispaa ya Ilala iliahidi kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti yake, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliamua kutengeneza barabara hiyo kwa awamu kwa kiwango cha lami kadri fedha zilivyopatikana. Awamu ya kwanza ilianza mwaka 2003/2004 na ilihusu kipande cha kilomita mbili kutoka Bima hadi Mawenzi kwa Masika ambacho kimekamiliwa na kiligharimu kiasi cha shilingi milioni 478.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilala inatafuta fedha za kukamilisha awamu ya pili yenye urefu wa 2.8 kutoka Mawenzi hadi Tabata Kisiwani ambayo itagharimu kiasi cha shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Ilala iliweza kurekebisha sehemu korofi zilizoharibika za barabara kutoka Mawenzi hadi Tabata Kisiwani ili ziweze kuendelea kupitika. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 barabara ya Kisukuru hadi Mawenzi imepangiwa kiasi cha shilingi milioni 15 kutoka fedha za Mfuko wa barabara kwa ajili ya kutengeneza sehemu korofi kwenye barabara hiyo ili iweze kupitika vizuri.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa 6 Serikali imekuwa inasema haina fedha.

(a)Je, ni lini itapata fedha hizo ili itengeneze barabara?

(b)Kwa kuwa wananchi wa Kisukuru wana uhakika master plan ya eneo hilo ilichezewa kienyeji hivyo kupitisha barabara mahali ambako haiko kwenye *master plan*, Serikali itakuwa tayari kwenda kuchunguza tatizo hili ilimalize na waliocheza nayo wachukuliwe hatua ili wananchi wa Kisukuru wapate barabara ya kisasa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Msindai hajaeleza huko Kisukuru sijui kuna nini? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA: Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwamba bajeti ambayo inahitajika kwa ajili ya kukamilisha hii barabara ambayo tumezungumza hapa ni zaidi ya bilioni 2 za Kitanzania na fedha hizi zinatakiwa ziwe zinapatikana kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ilala. Ni ukweli usiopingika kwamba hata kama wangechukua hela zote ambazo zimetolewa kwa ajili ya bajeti ya mwaka mzima hela hizo hazitatoshereza kwa ajili ya kutengeneza barabara.

Naambiwa na *TANROADS* wanazungumza habari ya kila kilomita moja huchukua zaidi ya shilingi milioni 450 hadi 500 kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba hela hizi zitapatikana lini, hela hizi zitapatikana wakati huo tutakapokuwa tumeleta hapa Bungeni na kupitisha na kusema hizi ndizo hela ambazo zimepangwa kwa ajili ya hiyo barabara tunayozungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, hicho ndicho ninachoweza kusema hapa kwa sababu tunaendeshwa hapa na Bajeti.

La pili, Mheshimiwa Mgana Msindai anasema kwamba barabara hii *master plan* imechezewa na kwamba angetaka kujua kama tutakuwa tayari kufuatilia jambo hilo na kama hatua zitachukuliwa kwa wale ambao wamechezea *master plan* hiyo.

Taarifa nilizo nazo ni kwamba barabara hii inapita hapa ambapo inatakiwa kupita lakini kwa vile Mheshimiwa Mbunge ni mtu ambaye ana taarifa nyingi sana siwezi kumpuza hapa. Mimi nataka niahi kwa niaba ya Serikali kwamba tutakuwa tayari kufuatilia hilo analolizungumza na kama ikidhihirika kwamba ipindishwapindishwa basi tutalifanyia kazi kama ilivyoelekezwa hapa. (*Makofi*)

SPIKA: Tusikie kutoka Ilala sasa.

MHE. MUSA ZUNGU AZZAN: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la barabara siyo la Tabata tu katika Mkoa wa Dar es Salaam. Dar es Salaam nzima barabara zake siyo nzuri na namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hivi karibuni ameweka

Tume ya kutazama Dar es Salaam ili iweze kutawalike. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuboresha miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam ili Mkoa sasa uweze kupitika na uweze kuwa na uwezo wa kukusanya mapato ili kusaidia mapato ili kusaidia Mikoa mingine? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA: Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nimshukuru Mheshimiwa Azzan Zungu, kwamba ametusaidia kuhusu taarifa hii ambayo ameitoa.

Ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelezo kwamba tufanye utafiti wa kutosha kuona kwamba barabara zetu za Dar es Salaam ma miundombinu yote iliyoko Dar es Salaam inapitika. Kama ninakumbuka vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe alisimama hapa na akasema kwamba kama tutatumia Bajeti hii ambayo tunatenga kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam haitawezekana kabisa kuweza kurekebisha miundombinu iliyoko Dar es Salaam. Iko kamati ambayo imeundwa kwa ajili ya kushughulikia na kutoa ushauri kwa Serikali namna gani tunaweza kusaidia Jiji la Dar es Salaam ili tuweze kulisaidia na matatizo haya ambayo Mheshimiwa Zungu yaweze kutatuliwa. (*Makofi*)

WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii ya kutoa maelezo ya ziada juu ya jibu zuri ambalo Mheshimiwa Mwanri amelitoa kwamba Serikali tayari inalifanyia kazi suala hili na *TANROADS* pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam. Sasa hivi wameshaainisha barabara zile ambazo zikifanyiwa kazi ndani ya mwaka huu wa fedha zitaleta maboresho makubwa na nafuu katika msongamano wa magari na hivi sasa tunachambua zipi ambazo tutaanza kuanza nazo kwa ajili ya upanuzi na pia ujenzi wa barabara mpya kwa mfano barabara inayotoka makutano ya Kigogo na kuja mpaka maziwa na kuja kuungana na barabara kuu ya Morogoro sehemu ya kituo cha basi. Kwa hiyo, kazi imeshaanza mchanganuo umeshafanywa na tutafanya marekebisho katika Bajeti ya mwaka huu wa fedha ili tuweze kuzifanya kazi hizo ndani ya mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Na. 87

Majengo ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA aliuliza:-

Kwa kuwa tangu kuundwa kwa Wilaya ya Mbinga miaka ya 1960 hakuna Ofisi ya Mkuu wa Wilaya:

- (a) Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo?
- (b) Kwa kuwa sasa ni kama miaka 45 imepita tangu kuundwa kwa Wilaya ya Mbinga. Je, Serikali itajenga lini Makao Makuu ya Wilaya hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Makao Makao ya Wilaya ya Mbinga yapo mahali ilipo ofisi anayotumia Mkuu wa Wilaya ya Mbinga hivi sasa. Jengo hilo linatumika kwa pamoja kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, ofisi hizo ziko katika Kiwanja Na. 1 ambacho kinajulikana kwa jina la Boma tangu mwaka 1965 na majengo yalijengwa mwaka huo ilipoanzishwa Wilaya ya Mbinga. Mmiliki wa halali wa kiwanja hicho hakuna kwa kuwa hakuna mwenye hati miliki baina ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa.

Majengo yote yaliyopo yamejengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mwaka 1965.

(b)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni miaka 45 tangu kuundwa kwa Wilaya ya Mbinga. Hata hivyo, pamoja na ofisi hizo kuwa pamoja hakujawahi kutokea malalamiko au mgogoro kati yao katika matumizi ya majengo hayo. Hivyo naomba kushauri kwamba kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga inaona kuwa inahitaji majengo ya ofisi dhidi ya hayo yaliyopo ianze mchakato wa taratibu za ujenzi kupitia vikao halali vya Wilaya na Mkoa.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Serikali imekubali kwamba majengo yale ni mali ya Halmashauri ya Mbinga na jukumu la kujenga Makao Makuu ya Wilaya kwa maana ya jengo la *DC* ni kazi ya Serikali Kuu.

(a)Je, sasa ni lini Serikali inaweza kutenga fedha katika Bajeti ya Serikali ili ijenge ofisi hiyo?

(b) Hadi sasa ni kweli mgongano haujatokea tangu *DC* na Mkurugenzi wakae hapo. Sasa Serikali inasubiri mpaka mgongano utokee ndipo ijenge ofisi hiyo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA: Mheshimiwa Spika, suala la ni lini ofisi hii itajengwa ni suala ambalo linahusu Wilaya ya Mbinga yenyewe. Mpaka asubuhi nilipokuwa nakuja hapa nilikuwa natafuta kuona kama kumekuwa kuna maombi yoyote yale au Bajeti yoyote ile ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga na taarifa nilizonazo ni kwamba hakukuwa kuna kitu cha namna hiyo.

Lakini kama nilivyojibu hapa kama Mheshimiwa Komba anaona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo ni kweli kabisa kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo ni kweli kabisa kwamba jambo hili haliwezi kuanzia kutoka huku juu liende kule chini, litaanzia kule chini kwa maana ya kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga pamoja na vikao vya Vikao vya Mkuu wa Wilaya yaani *DCC* vitakutana na kuona kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha jambo hili. Likija litafuata taratibu zake kupitia *Regional Consultative Committee* na kuweza kufika katika hatua hii.

Mheshimiwa Spika, la pili. Kwamba tunasubiri mpaka mgogoro utokee hapa, serikali inafanya kazi kama baba kama ukikaa ukasema mimi sina shati, baba atachukua hela atakwenda kununua shati atakupatia. Sisi mpaka sasahivi hatujasikia kwamba kuna tatizo lolote kwa hao kukaa wawili pale Halmashauri ya wilaya ya Mbinga kukawa na Mkuu wa Wilaya tuliona kwamba ina *harmonise*, tukaona kwamba kwa kukaa panmoja labda inaleta ufanisi zaidi. Lakini sasa inavyoonekana hapa inaonekana kwamba kuna tatizo pale kwamba Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna umuhimu wa kuwa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Hili hatuna ubishi nalo utaratibu huo niloueleza hapo ukishaafikiwa ukiletwa tutalishughulikia kwa taratibu hizo zilizowekwa. (*Makofi*).

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, wilaya ya Mbinga wananchi wake wanawakilishwa na Mheshimiwa *Captain* Komba, Mheshimiwa Gaudence Kasian Kayombo na Mheshimiwa Manyanya; na kwa kuwa, wakati nikichangia katika Bajeti ya *TAMISEMI* mwaka 2007/2008 suala hili pia nililiwakilisha kwa Serikali wakati huo akiwa Mheshimiwa Pinda, ambaye sasa ni Waziri Mkuu; na kwa kuwa, pia nilipochangia mwaka 2008/2009 suala hilo pia lililetwa mbele ya Serikali. Je, Serikali sasa iko tayari na wakati huo wote walikubali kwamba wataliweka katika Bajeti ya mwaka 2009/2010. Je, Waziri sasa yuko tayari kuwathibitishia wananchi wa Mbinga?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI WA MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Kayombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba inawezekana kabisa kwamba anaweza ikawa amelizungumza humu ndani. Na ile ripoti ambayo niliitoa hapa sikwenda kwenye *hansard* na kusoma *hansard* zote kuona kama limewahi kuletwa.

Lakini ninachozungumza hapa nazungumzia ule utaratibu ambao unatumika katika kuipata sasa pesa ambayo itakwenda sasa kujenga ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Jambo hili haliwezi kuanzia hapa Bungeni na wala haliwezi kuanzia kule, huwezi kuchukua tu hotuba ya Mbunge pale ukasema kwamba utakwenda kuifanyia kazi. (*Makofi*)

Ninachomwomba Mheshimiwa Kayombo, ni kwamba warudi sasa wakae katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na vile vikao vingine ambavyo nimezungumzia

ambavyo Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Wilaya, walizungumzie jambo hili na walipitishie katika Halmashauri ile ya ushauri ya mkoa wa Ruvuma na lije ili sasa sisi kwa pamoja tuweze kuliangalia jambo hili na liweze kuwa *reflected* katika Bajeti yetu.

Na. 88

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Mazingira inajitahidi kuweka nchi yetu kwenye sura nzuri ya usafi wa mazingira kwenye maeneo yote, na kwa kuwa, kumekuwa na tabia ya kutupa taka hovyoyote na kwenda haja ndogo au kubwa hovyoyote vitendo ambavyo havitakiwi kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira:-

(a)Je, ule utaratibu wa mabasi kuweka vifaa maalum vya kuwekea takataka utaanza kuekelezwa lini kuepuka hali ya abiria kutupa takataka hovyoyote njiani?

(b)Je, ni lini ule utaratibu wa mabasi kusimama njiani ili abiria watoke kufanya haja ndogo au kubwa kwa kisingizio cha kuchimba dawa utakatazwa?

(c)Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kutoa ilani ndani ya mabasi kukataza vitendo hivyo na badala yake waelekezwe utaratibu unaofaa kufuatwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS, MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na vitendo vya uchafuzi wa mazingira kama anavyoelezea Mbunge, vinavyofanywa na watumiaji wa vyombo vya usafiri hususan vyombo vya usafiri vitumiavyo barabara kuu kamavile mabasi, treni na magari makubwa.

Vilevile ni kweli kabisa vitendo hivyo si vya kistaarabu na havitakiwi kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na kanuni ya afya kwa ujumla. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeanza jitihada za kudhibiti tatizo hili. Hii ni pamoja na udhibiti wa taka kwenye vyombo vya usafiri na usafirishaji nchini.

Katika jitihada hizi, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, NEMC, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kabu na Majini, SUMATRA, wamezindua kampeni na kuanzisha rasmi udhibiti wa taka kwenye vyombo vya usafiri hasa mabasi yaendayo mikoani. Aidha, SUMATRA ilitoa matangazo kupitia

magazeti mbalimbali ikiwaagiza wamiliki wa mabasi kuhakikisha wanaweka vyombo vya kutupia takataka ndani ya mabasi ili kuepusha utupaji taka hovyoy.

(b)Mheshimiwa Spika, kupitia Sheri ya *SUMATRA*, Sheria Namba 9 ya mwaka 2001, *SUMATRA Act No. 9 of 2001*, Mamlaka iliandaa Kanuni inayohusu Viwango vya Ubora wa Magari pamoja na Huduma, *The SUMATRA Technical Safety and Quality of Service Standards, Passenger Vehicles, Rules, 2008*.

Katika kanuni hiyo ambayo ilitangazwa kupitia Gazeti la Serikali Namba 14 la tarehe 08/02/2008, kupitia kifungu namba 18 cha Kanuni hiyo, wasafirishaji wameagizwa kuhakikisha kuwa abiria wanapanda mabasi au wanapumzika na kujisaidia katika vituo ambavyo vina huduma muhimu kama vyoo, vivuli vya kupumzikia na huduma za vinywaji na vyakula.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza katika jibu langu la sehemu (a) *SUMATRA* tayari imekwisha waagiza wamiliki wa mabasi kuhakikisha wanaweka vyombo vya kutupia takataka ndani ya mabasi ili kuepuka utupaji taka hovyoy.

Sambamba na hilo, imeweka ilani inayowaelekeza abiria kutotupa taka hovyoy. Pamojana juhudi hizo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, *NEMC*, linaendelea na kampeni ya udhibiti wa taka pamoja na kutoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya *SUMATRA* kutoa maagizo kwa wamiliki wa vyombo hivyo. Je, imefuatilia kuona kwamba kuna utekelezaji wowote?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS, MAZINGIRA:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba suala hili kwanza liliulizwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, tarehe 21 Agosti, 2008 na katika majibu yake Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, alieleza jitihada za makusudi ambazo zinafanywa na Wizara

yake na kupitia wakala wake wa *SUMATRA* katika kudhibiti tatizo hili la kutumia na kufanya uchafuzi katika maeneo mengi ya barabara zetu.

Kwa hiyo, sasa hivi tayari Wizara imeshaweka vituo mbalimbali katika barabara kuu za kuweza kuwa na huduma za vyoo, lakini pia usimamizi unafanywa kwa kushirikiana na *SUMATRA* na *NEMC* kwa kupitia wakala ambao tayari sasahivi wameshaanza kusajiliwa, wale ambao watakuwa ni ma-*inspector*, wakaguzi wa mazingira ambao watapita katika maeneo mbalimbali. Tayari tumeshawasajili wakaguzi 30 lakini ni jitihada za Serikali kuwa na wakaguzi wasiopungua 200.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu masharti ya Kanuni. Wengine mnashindwa kunong'ona mnapiga kelele kabisa, si jambo zuri na wala halipendezi.

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ni zamu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Dr. Chrisant Mzindakaya, wa Kwela. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 89

Meli ya Liemba

MHE. ANNA R. LUPEMBE K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA aliuliza:-

Kwa kuwa Meli ya Liemba ndio meli pekee ya zamani duniani inayofanya kazi.

Je, Serikali haioni kuwa meli hiyo ingefaa kuwa kivutio kikubwa cha utalii?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Liemba ni meli inayofanyakazi katika Ziwa Tanganyika chini ya *Marine Services Company Limited* yenye Makao Makuu Jijini Mwanza. Meli hiyo iliundwa huko Ujerumani mwaka 1913 na kusafirishwa kwa Reli ya Kati katika awamu tatu, tarehe 19 Desemba, 1913 tarehe 12 Januari, 1914 na tarehe 27 Januari, 1914. Hatimaye meli iliunganishwa na kujaribishwa tarehe 8 Juni, 1915.

Meli hiyo ina historia kubwa ikiwemo kupigwa bomu na kuzama mwaka 1916 wakati wa vita kuu ya Kwanza ya Dunia. Meli hiyo iliibuliwa mwaka 1924 wakati wa utawala wa Waingereza na bado inafanyakazi hadi leo na ni usafiri unaotegemewa sana katika Ziwa Tanganyika.]

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa meli ya Liemba inaweza kutumika kama kivutio cha utalii.

Hivi sasa ratiba za ziara za watalii wanaozuru Magharibi mwaka Tanzania zinajumulisha pamoja na maeneo mengine, hifadhi ya taifa ya Gombe, hifadhi ya taifa ya Mahale, maeneo ya Kumbukumbu ya Dr. David Livingstone ya Ujiji na meli ya Liemba.

Aidha, kuna watalii wengi wa Kijerumani wanaofika Kigoma kuangalia meli hii. Kwa kutambua umuhimu wa malikale katika utalii, Wizara imeanza mchakato wa kujenga hoja ili *UNESCO* iitambue njia kuu ya watumwa, *slave route*, inayoanzia Ujiji hadi Kigoma mpaka Bagamoyo kuwa ni eneo la urithi wa dunia, *World Heritage Site*. Sambamba na hilo, Oktoba mwaka 2009 Tanzania itakuwa mwenyeji wa Kongamano la kitaifa linaloitwa, *African Diaspora Heritage Trail*, ambalo suala la njia kuu ya watumwa kutoka Kigoma hadi Bagamoyo ni mojawapo ya vielelezo vya kongamano hili. Ni matarajio yetu kuwa utambuzi wa njia hii kwa maana ya utalii kutatoa fursa kwa meli ya Liemba kujulikana zaidi na pengine kuwezesha wazo la kutumia kama kivutio cha utalii kupewa msukumo stahiki.

Mheshimiwa Spika, aidha katika kuendeleza wazo hili zuri, Wizara yangu itawasiliana na Wizara husika pamoja na mmiliki wa meli hiyo ya zamani ili kuona uwezekano wa kutumika kama zao la utalii kwa kuwa hivi sasa meli hiyo bado inaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

SPIKA: Kuna tangazo muhimu. Waheshimiwa Wabunge, kutakuwa na Orodha ya Shuguli ya nyongeza, *Supplementary Order Paper*, kwa ajili ya Azimio lile maalum. Lakini kwa sasa hivi nawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, waende kule kwenye Ukumbi wa Spika. Rasimu ya Azimio iko tayari. Na Kanuni inahitaji kwamba shughuli yoyote ni lazima ipite kwenye Kamati, hasa Azimio. Kwa hiyo, tunawaomba muende huko ili murejee baada ya muda mfupi ili Mwenyekiti Mheshimiwa Masilingi, aweze kuwa tayari na azimio na baada ya maswali na matangazo na Kauli ya Waziri na Uchaguzi, tuweze kulishughulikia Azimio husika. (*Makofi*)

Swali la nyongeza Mheshimiwa Anna Lupembe.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Sasa hii meli kwa muda huu inapoteza ratiba yake kabisa kutokana na hali ambayo sio nzuri ya meli. Meli ile sasa hivi tayari imeshakuwa mbovu. Je, Serikali sijui ina mipango gani ya kuiimarisha hiyo meli ambayo ndiyo meli ya kwanza ya kitalii katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kununua meli nyingine ya kutoka Kigoma kwenda Zambia? Maana meli ikitoka Kigoma inatusaidia sisi wananchi wa Mpanda Kikalema, Wilaya ya Nkasi, Kalambo, Kasanga mpaka Zambia. Je, Serikali ina mpango gani wa kutunulia meli mpya?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya dada yangu Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum. Na pengine kabla ya kujibu maswali yake naomba nimshukuru sana kwa kutambua jitihada ambazo Wizara inafanya na pia kwa mchango wake ambao anautoa kwa maendeleo ya wananchi wa Mkoa wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali halisi ya meli hii ni kweli hali yake si nzuri lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba meli hii baada ya kuwa imetoka kwenye iliyokuwa *TRC* na kuundwa kwa hiki chombo kinachoitwa *Marine Services Tanzania Company Limited*, sasa iko kwa mmiliki mpya ambaye tunaamini kwamba ataongeza nguvu katika kuimarisha meli zilizokuwa za *TRC*. Kwahiyo ninaamini kwamba kampuni hiyo ambayo ni changa chini ya Wizara ya Miundombinu wana mpango wao mkakati wa kuimarisha meli zilizopo ikiwa ni pamoja na wazo hili la pili la kununua meli nyingine.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Na mimi nina swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nipende kupongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba ni kweli *literature* au fasihi ya *MV. Liemba* imeandikwa vizuri kwenye Makumbusho ya *Dr. David Livingstone* pale Ujiji. Lakini palepale Ujiji panajengwa jumba kubwa la Makumbusho ambalo bilashaka *literature* zote zitahamishiwa kwenye jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua kwasababu jengo hili linajengwa na Wizara na limeanza kujengwa mwaka 2003, ni lini jengo hili sasa la kisasa la Makumbusho litakamilika pale Ujiji katika Mkoa wa Kigoma?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la nyongeza la Kaka yangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara inafanya mkakati wa kuboresha vivutio vya utalii hasa vilivyoko katika Idara ya Mambo ya Kale ikiwemo jumba la Makumbusho lililoko Ujiji. Mpango wa kuboresha jumba hili uko katika hatua za mwisho za utekelezaji ilikuwa tuwe tumemaliza katika mwaka huu wa fedha lakini kutokana na mambo ya kibajeti, hatukuweza. Kwa hiyo ni matumaini yetu kwamba mwaka ujao wa fedha tutakuwa tumemaliza kwasababu lengo letu ni kwamba tutakapokuja kuanza kuitangaza njia ya kati ya utumwa basi jengo hilo pamoja na vituo vingine vya utalii *along that route* viwe vimekamilika.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amevitaja vivutio vingi ambavyo viko katika Ukanda wa Magharibi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya ngome ya Bismark iliyoko kule Kasanga, iliyojengwa na wajerumani sambamba na ujenzi wa meli ya *MV. Liemba* kuwa ni kivutio cha utalii na kuanza kutumika kwa shughuli za utalii tu pekeyake?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mkoa wa Rukwa una vivutio vingi ikiwemo ile Ngome ya Bismark. Kwa muda mrefu Wizara imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuhifadhi maeneo ya kihistoria, lakini nguvu ambazo zimekuwa zikitumika kuvitangaza vivutio hivyo au vituo hivyo kama sehemu ya biashara ya utalii imekuwa si kubwa sana. Sasahivi tuna mpango mkakati wa kuboresha na kuongeza idadi ya vivutio vya utalii ikiwa ni pamoja na mambo ya mali ya kale.

Tunatumaini kwamba tutakapokuwa tumeboresha mawasiliano upande wa Magharibi mwa nchi yetu ikiwa na kuwepo kwa barabara ya uhakika kutoka Sumbawanga hadi Mbeya, maeneo hayo pamoja na mengine ya kitalii yakiwemo wanyamapori na mambo ya Gombe huko yataweza kutangazwa ipasavyo.

Kwa sasa hivi imekuwa ni tabu kidogo kwa sababu nguvu ambazo zimekuwepo kwenye eneo hilo ni kidogo. Lakini pia hata miundombinu ya upande huu imekuwa si nzuri sana.

Na. 90

**Ujenzi wa National Traditional
Medicine Laboratory**

MHE. GUIDO G. SIGONDA K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA
aliuliza:-

Kwa kuwa, dawa za asili zinachangia katika kutibu baadhi ya maradhi hapa nchini na kwamba Serikali inatambua hilo na imeamua kujenga maabara itwayo, *National Traditional Medicine Laboratory*, Jijini Dar-es-Salaam:-

- (a) Je, ujenzi wa kituo hicho ulianza lini?
- (b) Je, ni kitu gani kinakwamisha kukamilika kwa kituo hicho?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo kuhusu maabara hii ya dawa asili. Jina sahihi la maabara hiyo inayojengwa itaitwa, *Mabibo Traditional Medicine Laboratories*. Mkataba wa ujenzi wa maabara hiyo ulisainiwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 kati ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, *NIMR*, na mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa maabara hiyo imekadiriwa kugharimu shilingi 1,496,125,298.28/=. Mpaka sasa jumla ya shilingi 487,488,389.20/= zimekwishalipwa na Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo hicho ulianza tarehe 3 Juni, 2006, chini ya ukandarasi wa kampuni ya *NANDRA ENGINEERING & CONSTRUCTION LTD* na msanifu wa majengo *LANDPLAN-ICON ARCHTECTS LIMITED*.

(b) Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa ujenzi wa kituo ulikwama kutokana na ufinyu wa Bajeti na hivyo kupelekea kuchelewa kwa malipo. Hii ilisababisha kazi hii kusimama kwa muda kuanzia tarehe 1 Februari, 2008.

Hata hivyo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekwishalipa kiasi cha 300,000,000/= kwa mkandarasi na kwa sasa ujenzi umekwishaanza tena kuanzia tarehe 1 Septemba, 2008.

MHE. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, malengo ya maabara ni pamoja na kubaini na kuthibitisha aina za dawa kwa ajili ya kutibu aina ya magonjwa mbalimbali. Hivisasa kumejitokeza matangazo chungu nzima katika vyombo vya habari vinavyotangaza aina ya dawa zinazoweza kutibu binadamu ikiwa ni pamoja na kuongeza nguvu za mwili na hasa kwa

wanaume. Je, hizo dawa zimethibitishwa kwamba ni kweli zinaweza zikatibu hayo magonjwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Hao wanaotangaza hizo dawa wengi wanajiita ni madaktari, sasa sijui kitaaluma Wizara imekwisha wathibitisha hao madaktari kwamba kweli ni wauguzi ambao wana sifa za kiuguzi kitaaluma?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Sigonda, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna matangazo ya watu wanaojidai kwamba wanaweza kutibu hasa magonjwa sugu ambayo yanasumbua sana watu. Na matangazo ambayo hayajapata kibali cha Wizara ni matangazo ambayo yanakwenda kinyume cha sheria. Na Mheshimiwa Sigonda, atakuwa anajua kwamba tuna kitengo maalum kinaitwa *TFDA* na labda ana uhusiano nacho kwa karibu ambacho wanafanya kazi usiku na mchana kufuatilia masuala haya. *Ki-medical* huruhusiwi kujitangaza, hata ukiwa na dawa ni lazima ithibitishwe na inaandikwa kwenye majarida ambayo wataalamu wengine wanaweza wakayafuatilia. Kwahiyo tunayo orodha ya watu ambao tumewakamata, tunazidi kuelimisha watu kwamba wasinunue dawa hizi za mitaani na hata hapa tumewahi kuzungumzia habari ya dawa za kichina ambazo wanaingiza mpaka kwenye mabasi, ni kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, swali la pili lilikuwa ni kuhusu madaktari, kwamba hawa je, ni madaktari? Nasema sio madaktari; madaktari tunayo orodha yao, lakini hakuna sheria ambayo inamkataza mtu kujipa cheo cha namna hiyo. Sasa kwa bahati mbaya basi inawalaghai watu na wanataka waamini kwamba wale kweli ni watu waliokubuhu, na hii tena ni kinyume na sheria.

SPIKA: Kabla Mheshimiwa Susan Lyimo, hajauliza swali la nyongeza, nimepata fununu kwamba wapo humu wengine nao wanajiita madaktari na wakati sio. Kwa hiyo kidogo ni hatari. Kumbe ni kinyume cha sheria, mimi sikujua hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na kwamba swali langu kidogo lingefanana na la pili lakini ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri na pia niliwahi kumuuliza kwenye Kamati. Kwa kuwa, wengi wa waganga hawa wa kienyeji au wa asili wamekuwa na hizi dawa na wamekuwa wakizitangaza hadharani. Kwa mfano wanasema kwamba wanatibu *UKIMWI*, wanatibu kisukari na magonjwa mengine ambayo kisayansi yameshathibitika kwamba hayatibiki.

Je, sasa Serikali inasema nini, inatoa tamko gani kwa watu hawa? Kwasababu kwa kweli wananchi wengi wamekuwa wanapoteza fedha zao bila ya mafanikio yoyote. Serikali inasemaje sasa kwa watu hao?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna watu ambao wanajidai wanaweza kutibu haya magonjwa ambayo kisayansi tunajua kwamba hayatibiki na ni kweli kwamba Mheshimiwa Susan Lyimo, amewahi kuniuliza hili swali. Na ametoa mfano wa ugonjwa wa *UKIMWI* lakini pia naomba nimrejeshe wakati tunapitisha sheria ya kudhibiti *UKIMWI* hili suala lilijitokeza na kauli ilitolewa ambayo iko kwenye sheria kwamba ni kinyume na sheria.

Kwa maana hiyo mtu atakayefanya hivyo anakwenda kinyume na sheria na sasahivi kanuni zinaandikwa za namna ya kuwabana na kuwafikisha mbele ya vyombo. (*Makofi*).

Na. 91

Ushindani wa Makampuni ya Simu Tanzania

MHE. HAROUB SAID MASOUD aliuliza:-

Kwa kuwa, ushindani wa Kampuni za Simu Tanzania umeongezeka kiasi ambacho unasababisha njia za simu zigawiwe mitaani bure.

(a)Je, Serikali haioni kuwa mteja kupewa njia ya simu bila kufanyiwa usajili kunahatarisha utulivu?

(b)Je, kwa nini Serikali haitungi Sheria itakayozibana kampuni hizo kutoa njia bila usajili kama zinavyofanya baadhi ya nchi?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa pamoja na manufaa makubwa ya huduma za simu katika kuharakisha Maendeleo ya kijamii na kiuchumi, simu hizo zinapotumika isivyo sahihi, huweza kusababisha athari kubwa na hivyo kuhatarisha utulivu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/2009 kuwa Serikali itaanzisha rejesta, *Central Equipment Identification Register – CEIR*, ili kudhibiti matumizi mabaya ya simu za kiganjani kwenye aina yoyote ya mtandao nchini na nchi za Afrika Mashariki. Serikali imeanza kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa matumizi ya simu hizi hususan kurejea utaratibu wa sasa wa kuuza na kusambaza holela laini za simu, *simcards*.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, TCRA, iliunda Kamati ya Kitaifa iliyojumuishia Makampuni yote ya simu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi ya Uhamiaji, Ofisi ya Mamlaka ya Mapato na Idara mbalimbali ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano kuweza kuangalia kwa undani njia muafaka zitakazoweza kupata na kutunza kumbukumbu za majina na anuani za watumiaji wote wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti usajili wa *simcards* na simu, *hand sets*, makampuni yanatakiwa yawe na mtambo wa kusajili na kubaini simu zinazotumika, *Central Equipment Identification Register*. Hivyo basi mtambo huu utakuwa na uwezo wa kuitambua simu na mmiliki wake. Faida ya mtambo huu itakuwa ni pamoja na:-

1. Kusaidiwa kutambua na kudhibiti wizi wa simu;
2. Kuzuia matumizi mabaya ya simu na kuzuia uhalifu;
3. Itasaidia upatikanaji wa ushahidi katika matukio yatokanayo na matumizi mabaya ya simu; na
4. Sheria hii itasaidia kubaini kiurahisi mtandao wa matukio yanayohusisha teknolojia ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inapitia sheria ya sasa na kupendekeza sheria mpya ili kuhakikisha kwamba sheria mpya inakwenda na wakati kulingana na mabadiliko ya teknolojia ya karne hii. Sheria zitakazounganishwa ni:-

- Sheria ya Mawasiliano Na 18 ya 1993, *Tanzania Communications Act. No. 18 of 1993*)
- Sheria ya Utangazaji Na. 6 ya 1993, *Tanzania Broadcasting Services Act. No. 6 of 1993*).
- Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Na. 12 ya 2003, *Tanzania Communications Regulatory Authority Act. No. 12 of 2003*, kuwa sheria moja ya mawasiliano kwa urahisi wa udhibiti na rejea.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu itahakikisha utekelezaji wa suala hili unaharakishwa ili mapema mwakani 2009 muswada wa marekebisho ya sheria hiyo uweze kuletwa bungeni.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa, sheria marekebisho ya sheria bado hayajawa tayari kuletwa hapa Bungeni na kwa kuwa matatizo ya simu yanazidi kuwa makubwa sasa nina maswali mawili yafuatayo;

Je, ni nani atakuwa dhamana wa ndoa iliyotenganishwa kwa mume au mke ambao wanapelekwa meseji za mapenzi mabaya sana halafu baadaye mhusika akaitupa line hiyo ya simu?

Kwa kuwa, katika Bunge la 1995 – 2000 Wabunge wote wa Zanzibar na wa bara walipingania sana kampuni ya *ZANTEL* iweze ku-operate hapa Bara, lakini hivi karibuni kuna *promotion* ambayo kwa siku tano kwa wiki ambao wanafaidika watu wa Bara tu. Je, Watu wa Zanzibar wanaambiwa nini kuhusu *promotion* hii ambayo wao wanazalilika sana?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kuhusu meseji zinazotumwa kwenye simu na nyingine zinahatarisha hata ndoa, wala sio ndoa tu watu wengine wanatishiwa kuuwawa, watu wengine hata humu ndani wamekuwa wakipokea meseji za uchochezi wa kisiasa na mambo mengine. (*Makofi*)

Wakati sheria hii inatayarishwa kuna utaratibu ambao unaweza kutumika kwa kufuatilia ile namba ambayo imepigwa, ni njia ndefu kidogo nafikiri una *dial 000160* na kuendelea halafu hatimaye itakupeleka kwenye mitambo ukifuatilia unaweza kupata mtu aliyepiga. Kwa sababu ile itatambua hata ile *handset* ambayo imetumika.

Lakini hii tunayoileta itakuwa ni rahisi zaidi, kazi ya mtambo unaozungumzia si kwamba kutakuweko na mtu anasikiliza kila wakati, lakini *all discussion* mazungumzo yote yatakuwa yanakuwa *recorded* na mara mtu atakapolalamika itakuwa rahisi kufuatilia kwenye mtambo ule ambao utakuwa na *special soft ware*.

Kuhusu *ZANTEL* ambayo ina promotion Bara lakini hakuna promotion kama hiyo kule Zanzibar, nachukua hili suala halafu nitazungumza na kampuni inayohusika. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa *session* ya Bunge lililopita tuelielezwa na Naibu Waziri kwamba kuna athari kubwa ya matumizi ya muda ya simu za mkononi katika mfumo wa fahamu na kwa kuwa sasa kuna ushindani mkubwa wa kibiashara ya makampuni yote ya simu kuruhusu matumizi ya simu kuanzia saa 11 Asubuhi mpaka saa 12 jioni kuwa ndogo.

Je, Serikali haioni kwamba hii inaweza ikawa ni biashara haramu ambayo baada ya muda itawaacha watu na athari kubwa kiafya kuhusu mfumo wa ufahamu?

SPIKA: Ni moja tu, ni swali kwa sababu nyongeza haiwezi kuwa na maswali mawili.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla ambaye anauliza juu ya athari za matumizi ya simu kwa muda mrefu. Utafiti uliofanywa unaonyesha kwamba hayana athari kubwa kwa watumiaji.

Kuna mionzi inayoitwa *ionizing radiation* na *non-ionizing* samahani Spika sina Kiswahili kizuri kwa hayo. Lakini inayotumika kwenye simu zetu ni *non-ionizing radiation* ambayo haina madhara makubwa kwa mtumiaji.

Hata hivyo kama anayetumia simu, maana yake kutumia simu ni kupeleka meseji kuzungumza lakini wewe kama umeshikilia hapo kwa kweli kwa saa moja na zaidi ni lazima kuna sehemu fulani ya madhara kwa sababu ya *electro magnetic radiation* ile sauti unapozungumza vilevile kuna kuwa na *radiation* fulani ya mawimbi yale yanaweza kama unatumia kwa muda mrefu utaona hata simu imepata moto na wewe unaanza kutoa jasho.

Kwa kweli ushauri wangu watu watumie simu kwa kuzungumza kwa kupeleka meseji ambazo ni muhimu lakini wasitumie kwa muda mrefu mazungumzo ambayo hayana mambo muhimu. (*Makofi*)

Na. 92

Chuo Cha Ushirika Tawi la Kizumbi – Shinyanga

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA aliuliza:-

Kwa kuwa, Chuo cha Ushirika Moshi Tawi la Kizumbi Shinyanga, kilikuwa kinatoa elimu ya kiwango cha cheti, *Certificate Level*, tangu mwaka 1985 – 1995:-

(a) Je, ni sababu zipi zimesababisha Chuo hicho kisiendeleo kutoa kiwango hicho cha elimu baada ya mwaka 1995?

(b) Je, Bajeti kiasi gani kwa mwaka hupelekwa chuo Chuo cha Kizumbi tangu 2004/2007 na Bajeti hiyo hutumika katika shughuli gani?

(c)Je, ni nini kinakwamisha kulifanya tawi la Kizumbi kufanya sehemu ya Chuo Kikuu wakati eneo lake ni ekari 232 na kuna majengo mazuri ikilinganishwa na tawi la Moshi lenye ekari 78?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Emmanuel Jummanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli tawi la Kizumbi la Chuo cha Ushirika Moshi , halikuendelea kutoa mafunzo kwenye kiwango cha cheti baada ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo ulichukuliwa kufuatia mabadiliko yaliyofanyika katika Muundo wa Utumishi wa Kada ya Maafisa Ushirika ambao uliweka viwango vya kuingilia kazini katika utumishi wa Serikali kwa Maafisa Ushirika kuwa ni Stashahada badala ya Cheti. Hivyo wahitimu wa cheti ambao walikuwa wanaandaliwa katika Tawi hilo kwa ajili ya kuajiriwa na Serikali wasingeweza kuajiriwa tena kwa sifa hiyo.

Hata hivyo, Tawi hilo la Kizumbi limekuwa likiendelea na utaratibu wa kutoa mafunzo maalum ya *tailor made courses* ya muda mfupi kwa wanaushirika na wadau wengine.

Aidha, kutokana na mageuzi katika Vyama vya Ushirika, na hasa *SACCOS*, kutakiwa kuajiri watendaji wenye sifa, tayari Chuo Kikuu Kishiriki kimeanza tena kutoa mafunzo kwa ngazi ya cheti kwa kozi ya *Microfinance* kwa watendaji wa vyama. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, watendaji 35 walipata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha katika mwaka wa fedha 2009/2010, Chuo Kikuu Kishiriki kina mpango wa kuhamishia mafunzo ya cheti kuhusu *Microfinance* na *Cooperative Management* kwenye tawi la Kizumbi, baada ya ukarabati wa maktaba.

(b)Mheshimiwa Spika, tawi la Kizumbi la Chuo Kikuu Kishiriki Moshi limekuwa likipelekewa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa tawi jilo na mishahara kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2004/2005 – Shs 46.7 milioni
- Mwaka 2005/2006 – Shs 60.5 milioni
- Mwaka 2006/2007 – Shs 69.2 milioni
- Mwaka 2007/2008 – Shs 93.8 milioni

(c) Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara makao yake makuu ni Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Tawi la Kizumbi lililoko Shinyanga ni mojawapo ya matawi ya Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeza Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa, vijana wanaomaliza kidato cha nne sasa hivi ni wengi sana kuliko wale wanaoenda kidato cha tano na sita na kwa kuwa, Serikali imeonyesha nia ya kurudisha pale kiwango cha cheti.

Lakini imeonyesha mwaka 2007/2008 imechukua watu 35 tu na Serikali haioni kwamba kuondoa kiwango cha cheti na wakati wimbi la vijana wanaomaliza kidato cha nne ni wengi tutawafanya wabaki kijiji kuwa wakulima na hatimaye kufanana na darasa la saba bila msaada?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi tunarudisha mafunzo ya cheti kwa nia ya kusaidia Vyama vya Usharika. Vyama hivi ni SACCOS ambazo zinahitaji utaalum. Vilevile kuna vyama vya msingi vya mazao ambavyo vinahitaji kuajiri watu ambao wamesomeswa kwa fani hii.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba tutaendeleza mafunzo yale sio kwa ajili ya utumishi wa Serikali, lakini kwa ajili ya kusaidia mfumo wa Ushirika nchini.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kizumbi ni tawi kubwa kuliko matawi yote ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika cha Moshi na chuo kikuu hiki kishiriki cha Moshi kinatoa mafunzo ya Ushirika pekee Afrika. Ni lini Serika itakiwezesha chuo hiki kuanza ujenzi wa kitivo cha Ushirika na Usimamizi wa fedha katika kituo cha Kizumbi katika harakati za kukifanya chuo hiki kuwa Chuo Kikuu kamili kwa lengo la kuimarisha Ushirika nchini?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, chuo kikuu kishiriki cha moshi hakijawa chuo kikuu pekee ni kishiriki kwa hiyo kwa sasa hivi eneo linalozungumziwa litakuwa linaendelea kuwa sehemu ya chuo kikuu kishiriki na kitakuwa kinatoa mafunzo ambayo nimekwisha kuyaeleza. Lakini katika siku zijazo iwapo chuo hicho kitafanywa kuwa chuo kikuu peke yake na kikawa kinajiweza kwa Bajeti kupanuka hilo litaweza katika siku zinazokuja lakini kwa sasa eneo analolizungumzia tunalitumia kwa ajili ya mafunzo ya cheti kwa ajili ya kuboresha mfumo wa Ushirika nchini. (*Makofi*)

Na. 93

Upatikanaji wa Matrekta Maalum ya Kulimia Mpunga

MHE. CASTOR RAPHAEL LIGALAMA aliuliza:-

Kwa kuwa, mapinduzi ya kilimo cha mpunga katika nchi za Japan, Veitnam, Thailand, Indonesia na nyinginezo yamechangiwa na utumiaji wa matrekta madogo aina ya *Power Tiller* ambayo yanaweza kulima, kupiga haro na kuchangaanya:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuziwezesha Wilaya zote zinazolima mpunga kupata matrekta hayo kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu?

(b)Je, Serikali itakuwa tayari kugharamia mafunzo kwa maofisa Ugani na vikundi vya wakulima wadogo wadogo kwenda katika Chuo cha Mkindo Turiani, Morogoro kwa mafunzo ya vitendo ya jinsi ya kutumia matrekta hayo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Wizara inahamasisha matumizi ya matrekta madogo ya mkono hasa katika kilimo cha mpunga, kwa kuzingatia ukweli kwamba idadi kubwa ya wakulima wetu wanamiliki mashamba madogo madogo na kwa hali halisi, wengi wao hawawezi kumudu kumiliki matrekta makubwa ambayo bei yake ni kubwa.

Kuanzia mwaka 2003/2004, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo inatoa mikopo kwa wakulima kwa ajili ya kununua matrekta yakiwemo matrekta madogo ya mkono maarufu kwa jina la *Power Tiller*. Utaratibu unaotumika kupata mikopo hiyo ni kwamba, wakulima hutakiwa kuwasilisha maombi yao kwenye Mfuko wa Pembejeo kupitia katika Halmashauri zao. Hadi sasa, Mfuko umetoa mikopo ya matrekta ya mkono 84 yenye thamani ya TSh.441,895,000/=.

Wakulima wengi wadogo hawajaweza kunufaika na mikopo ya Mfuko kwa sababu ya kukosa dhamana.

Ili kuwezesha wakulima wengi wasio na dhamana ya mali isiyohamishika kupata mikopo hiyo, wanashauriwa kujiunga katika Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOs*), ambavyo vitaweza kuwadhamini.

Aidha vyama hivyo vitasaidia kujenga uwezo wa wakulima kukopeshwa na kununua matrekta ya mkono ambayo bei yake ni kati ya milioni 3.6 hadi 6. Serikali pia inaendelea kuhamasisha Taasisi mbalimbali za kifedha kama *PASS* na *SELFINA*, kuendelea kutoa mikopo ikiwemo ya matrekta madogo ya mkono.

(b)Mheshimiwa Spika, fursa kubwa iliyopo ya kugharamia mafunzo kwa maofisa ugani na vikundi vya wakulima ni kupitia kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) inayotekelezwa chini ya Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (*ASDP*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuisitiza kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepewa madaraka ya kupanga na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ikiwemo utekelezaji wa huduma za ugani. Serikali kuu inaendelea na jukumu la usimamizi wa sera, utoaji wa huduma za kitaalamu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji.

Wizara kupitia Chuo cha Mkindo pamoja na vyo vingine vya wakulima vya Bihawana (Dodoma); Inyala (Mbeya); na Ichenga (Njombe) iko tayari kutoa mafunzo kwa kutumia wataalam wake endapo Halmashauri za Wilaya zitatenga fedha kwenye mipango yao na kupeleka maafisa ugani na wakulima kupata mafunzo ya vitendo.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda nimshukuru Waziri kwa kutoa elimu kwa Halmashauri zetu jinsi ya kuwasaidia hawa wakulima wadogo. Nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wengi kwa sasa hivi wamehamasika sana na ununuzi wa matreka haya na kwa kuwa mfuko wa pembejeo sio mkubwa sana kuweza kukidhi kukopesha matrekta makubwa na madogo. Je, Waziri atakuwa tayari kumshauri Rais ili katika zile pesa kutoka EPA kwenda mfuko wa ruzuku ya mbolea kiasi iende kwenye mfuko ili mfuko uweze kutumika.

Kwa kuwa mikopo mingi ya mfuko wa mkopo huu utegemea sana mawakala ambao wamezagaa mjini wakileta aina mbalimbali za *matractor* hayo, kiasi ambacho nahisi kutakuwa na tatizo la vipuri. Je, kwanini mfuko wa Taifa wa pembejeo mfuko wenyewe ukaagiza matrekta hayo ili baadaye kusiwe na tatizo la vipuri na bei ya matrekta hayo ikaweza kudhibitiwa kuliko kutumia mawakala?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kuanzisha mfuko wa kukopesha wakulima kupitia mabenki au kupitia mfuko kwa kupitia fedha za EPA. Nadhani suala hili limeelezwa vizuri na Mheshimiwa Rais alipolihutubia Bunge kwamba fedha hizi sehemu yake itapelekwa katika benki ya Rasilimali ili kuanzisha dirisha au kwa ajili ya kukopesha wakulima.

Kwa hiyo, mimi nadhani sio lazima mkopo utoke katika mfuko ule wa pembejeo, lazima iwepo mifuko mingi zaidi ya kufanya kazi hii. (*Makofi*)

Vilevile uko mfuko mwingine ambao umeanzishwa kwa mkataba maalum na guarantee imewekwa na *USAID* yaani shirika la maendeleo la Marekani pamoja na benki ya maendeleo ya Afrika kupitia CRDB ambao na wao wamekubali sasa kutoa mikopo ya muda mrefu kwa kilimo, na kwa kweli kupitia *SACCOS* ambo CRDB wanazijua vizuri sana wakulima wanaweza kukopa matrekta madogo kupitia CRDB, wataendelea kukopa kutumia mfuko wa pembejeo na wanaweza kukopa kupitia dirisha la *TID* ambalo lilielezwa vizuri na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, kabla sijamshauri yeye alikwishaona tatizo hili na alishalieleza vizuri.

Swali la pili linalohusiana na wakulima na hizi trekta ndogo, tunachosema ni kwamba wakulima waendeleo kuomba mikopo hii wazitumie trekta hizi ndogo kwa

sababu ndiyo zinazoweza kuwasaidia wakulima wadogo na sisi Wizara tuko tayari kushirikiana nao lakini kwamba zinaingizwa trekta na wafanyabiashara hiyo ni katika mfumo wa soko uria, kwa sababu hatutaki tena ile benki iwe ukiritimba yenyewe tu ndiyo inayoagiza. Yenyewe ifanye kazi ya kutoa mikopo na wafanyabiashara wanaoweza kuingiza matrekta waingize isipokuwa tunayafanyia uchunguzi kupitia kituo cha *CAMATEC* ili kuwa na uhakika ya kwamba kweli yanafaa kwa matumizi ya ardhi yetu.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matumizi ya *tractor* haya ya *power tiller* yatawakomboa wakulima wetu kutokana na matumizi ya jembe la mkono lakini dhahiri shahiri vilevile kwa muda yatabadilisha maendeleo ya kilimo chetu ambacho sasa ni duni. Je, Serikali haioni umuhimu wa matrekta haya kuja kuwekezwa. Kwa maana ya kuunganishwa matrekta hayo hapa hapa nchini? (Makofi)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kuna umuhimu kwa kweli wa kuwatia moyo wawekezaji ambao wanaweza kuja kuunganisha matrekta hayo badala ya sisi kuendelea kuyaagiza. Wakati tulipotembelea huko Indonesia mwaka jana (2007) tulitembelea kiwanda cha namna hiyo na nilikuwa na Mheshimiwa Ligallama ambaye ameuliza swali hili na tulijaribu kuwashawishi watengenezaji wa Indonesia waje nchini. Vilevile tunawatia moyo watengenezaji wa nchi zingine watakaoweza kuja ili tuwape nafasi ya kuunganisha matrekta hayo hapa ili yawepo kwa wingi zaidi yaweze hata bei zake zikashuka panapokuwepo ushindani.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mtaniwia radhi nilimuona Mheshimiwa Ngasongwa kabla sijasema ni swali la mwisho kwenye kilimo, naomba nimpe nafasi sikumbuki yeye kuuliza swali la nyongeza kwa muda mrefu.

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii na ni kweli sijauliza swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali imefanya maamuzi ya kuiteua mikoa sita ndiyo itakuwa mikoa mikuu ya kuhimiza uzalishaji wa kilimo ili kujitosheleza kwa chakula, mikoa hiyo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Kigoma. Na kwa kuwa, benki *FBME* benki yaani *Bank of Federal, Federal Bank of the Middle East*, ina utaratibu tayari kwa kushirikiana na *DEMACO* ambayo ni kampuni binafsi inakopesha wakulima kupia *SACCOS* zako na watu wa Mkoa wa Morogoro wameshanufaika kwa matrekta kumi mpaka sasa je, Serikali inaweza sasa ikatenga baadhi ya fedha za *EPA* kuziweka katika benki hii ili zitumike kama guarantee kwa wakulima hawa?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba imeteuliwa mikoa fulani ili tuweke nguvu yetu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa chakula na hiyo mikoa sio sita peke yake iko zaidi. Ile mikoa sita anayoizungumzia ni ile ambayo ilikutana Mjini Morogoro hivi karibuni.

Lakini Kaskazini mwa Tanzania iko mikoa zaidi mingine. Iko mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na vilevile iko wilaya ya Tarime ambayo ina hali ya hewa inayofanana kabisa na mikoa ya Kusini nyanda za juu.

Kwa hiyo, kama mpango upo kwa ajili ya kusaidia basi tutafanya katika mikoa yote na vilevile suala la utoaji wa mikopo haliwezi vilevile kuelekezwa kwenye chakula peke yake kwa sababu kuna mikoa ambayo inazalisha mazao mengine na yenyewe inahitaji mikopo ya aina hiyo. Kwa hiyo tutaelekeza mikopo kwa nchi nzima sio kwa ajili ya mikoa fulani peke yake.

Na kuhusu suala la fedha za *EPA* mimi nadhani zilikwisha gawanywa sasa sijui tena tutazigawaje kwa kila benki lakini hili naliachia Waziri wa Fedha ambaye ndiyo msimamizi mkuu wa fedha hizi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa majibu yako.

Na. 94

Serikali Kupanga Ofisi Kwenye Majengo Binafsi

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali ilieleza kuwa bado Wizara na Taasisi nyingi zinaendelea kupanga Ofisi kwenye nyumba za watu binafsi:-

- (a) Je, ni Wizara na Taasisi ngapi na zipi za Serikali bado zinapanga ofisi kwenye majengo ya watu binafsi?
- (b) Je, Serikali hutumia kiasi gani cha fedha kwa mwaka katika kupanga ofisi hizo?
- (c) Je, ni sababu zipi zinazoifanya Serikali iendelee kupanga ofisi kwenye majengo hayo na kuna mpango gani wa kuondokana na hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambani, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu tulizonazo Wizarani jumla ya Idara na Taasisi nane (8) za Serikali ndizo katika maeneo mbalimbali nchini. Idara na

Taasisi hizo ni Idara ya Madini, Mahakama Kuu ya Ardhi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), Shirika la Posta, Benki ya Posta, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF). Pamoja na Idara/ Taasisi hizo za Serikali zinazopanga kwenye majengo ya watu binafsi. Zipo pia Taasisi za Wizara 19 zinazopanga katika majengo ya Mashirika ya Umma. Kwa vile orodha hiyo ni ndefu nitampatia Mheshimiwa Mbunge ili aipitie mwenyewe. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo hivi sasa, Serikali hutumia jumla ya Tshs. 12,540,000/= kwa mwezi kwa kupanga katika nyumba ama majengo ya watu binafsi na kiasi cha Tshs. 5,0981,104,517.52 kwa mwaka kwa kupanga katika majengo ya Taasisi/Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa malipo hayo umeunganishwa kwenye orodha inayoonyesha Idara/ Taasisi za Serikali zinazopanga majengo hayo.

(c) Mheshimiwa Spika, sababu kuu zinazofanya Serikali iendelee kupanga ofisi kwenye majengo ya watu binafsi ni kutokana na ufinyu wa bajeti ya kila mwaka, ambapo Serikali hushindwa kutenga fedha za kutosha kujenga majengo yanayohitajika kwa mara moja ukilinganisha na fedha inayotakiwa kupanga. Kwa mtindo huu wa kupanga, Serikali imeweza kulipa kiasi kidogo cha fedha kwa mwaka na hivyo kutoa fursa kwa Idara na Taasisi nyingine za Serikali kupata ama kutengewa fedha za kuweza kukidhi mahitaji mengine muhimu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga majengo ya Serikali kwa kutenga fedha kidogo kidogo kila mwaka ili kukidhi haja ya kuwa na majengo ya ofisi zake yenyewe. Lakini kama nilivyokwishaeleza, sehemu kubwa ya ofisi za Serikali zinazopanga ziko kwenye nyumba za Mashirika ya Umma ambazo zitaendelea kutumika wakati ujenzi wa ofisi za Serikali unaendelea kidogo kidogo.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Taarifa nilizonazo mimi ni kwamba baadhi ya idara na Wizara za Serikali hutumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kupanga majengo kwa ajili ya shughuli zake.

Mfano Wizara ya Viwanda na Biashara hulipa zaidi ya shilingi milioni 700 kwa mwaka kwa ajili ya kupanga katika jengo la *NSSF Water Front* pale Dar es Salaam. Lakini pia Mamlaka ya Hali ya Hewa hutumia zaidi ya shilingi karibu milioni 500 kwa ajili ya kupanga pale kwenye jengo la *Ubungo Plaza*, na Waziri ametueleza kwamba Serikali inatenga pesa kidogo kidogo kwa ajili ya ujenzi wa majengo haya. Haoni kwamba pesa tunazotumia kwa ajili ya kulipa kodi hizo hizo zingeweza kutumika kwa ajili ya kujenga majengo ya Serikali ili kuondokana na masuala ya kupanga katika majengo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, shirika la hifadhi ya jamii *NSSF* limekuwa hivi karibuni likitoa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga majengo mbalimbali ya Taasisi

mbalimbali za umma. Kwa nini Wizara isizungumze na *NSSF* ili itoe pesa ili zijenge majengo hayo ya Wizara na Idara za Serikali zinazopanga sasa ili kuondoka na utegemezi huo na kwa maana hiyo kufanya taasisi hizo ziweze kufanya kazi katika mazingira yaliyo tulivu zaidi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza juu ya baadhi ya Wizara zinazotumia fedha nyingi katika pango la ofisi nimesema hapa katika jibu la msingi ya kwamba kuendelea kupanga huko sio kwamba ndiyo tumefikia mwisho nimesema kwamba tutaendelea kutenga fedha kidogo kidogo ili kuweza kujenga majengo ya ofisi.

Kwa hiyo hizi taasisi ama Wizara zinazopanga katika majengo ya umma ama watu binafsi wanayo mipango tayari ya kuweza kujijengea majengo yao wenyewe.

Mimi nimekuwa katika Wizara ya Viwanda hivi karibuni nafahamu kabisa kwamba pale Wizara ya Viwanda wana mpango mahususi kabisa kutaka kushirikiana na mashirika yao yaliyoko chini ya Wizara kuhakikisha kwamba wanatujengea jengo la Wizara ambalo linaweza likachukua taasisi zote zilizoko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Kwa hiyo, mipango ipo lakini kama nilivyokuwa katika jibu la msingi ni kwamba uwezo tu wa kuchukua fedha zote katika kujengea majengo haya ndiyo unasita kidogo kwa sababu fedha hizo hizo zinatakiwa zitumike katika kutekeleza mipango mingine ya kitaifa ikiwemo ujenzi wa barabara, pamoja maji na kadhhalika.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kuitumia shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ni mpango mzuri ambao mimi kusema kweli nataka niungane na Mheshimiwa Mbunge. Lakini kama nilivyokuwa nimesema kwamba shirika hili pamoja na mashirika mengine yenye majengo hivi ndiyo yanasaidia kuzihifadhi ofisi zetu za Serikali.

Lakini ni mpango mzuri tu kama tutaweza tukashirikiana kiwizara pamoja na hizi taasisi zenye fedha. Mpango huo unaweza ukazungumzika na ukatekelezeka. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunatumaini ofisi mpya hiyo ya viwanda itajengwa Dodoma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali unakaribia kufikia ukomo, lakini ninadhani ni utaratibu mzuri tu tumalizie haya mawili mafupi ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa maana hiyo basi ninamwita Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, kwa swali linalofuata kwa niaba yake.

Zoezi la Urasimishaji na Makusanyo ya Ushuru

MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH (K.n.y. MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA) aliuliza:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika zoezi la urasimishaji ndani ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na katika utaratibu wa kuirejeshea SMZ makusanyo ya Ushuru wa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kuuzwa Zanzibar kama ilivyoelekezwa kwenye Bajeti ya 2007/2008?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilipatikana na bidhaa gani zilikusanywa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Jimbo la Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (*The Excise Management and Tariff Act, CAP 147*), yaliyofanywa mwaka 2007/2008 na kurasimisha utaratibu wa kuirejeshea SMZ makusanyo ya Ushuru wa Bidhaa zinazozalishwa Bara na kuuzwa au kutumiwa Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa haina msingi wa kisheria wa kuirejeshea SMZ makusanyo hayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imetekeleza maelekezo yaliyotolewa kutokana na mjadala wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2007/2008, kwa kurejesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar makusanyo ya ushuru wa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kuuzwa Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2007/2008, Mamlaka ya Mapato Tanzania, inafanya marejesho ya ushuru moja kwa moja kwa SMZ kupitia Mamlaka ya Mapato Zanzibar. Kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2007 hadi Septemba, 2008, Serikali ya Muungano kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, imeirejeshea SMZ jumla ya shilingi milioni 4,888.2 kupitia Mamlaka ya Mapato Zanzibar. Fedha hizo ni marejesho ya Ushuru wa Bidhaa unaotokana na bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kuuzwa Zanzibar.

Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 3,872.4 ni marejesho ya Ushuru wa Bidhaa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 na shilingi milioni 1,015.8 ni kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2008/2009 (Julai – Septemba, 2008). Bidhaa zilizohusika na marejesho ya Ushuru huo ni Sigara, Bia, Pombe Kali na Soda.

MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa nataka kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makampuni ya simu ambayo yanafanya kazi Tanzania nzima, hufanya pia kule Zanzibar, lakini mengi ya makampuni hayo yanalipia kodi zao hapa Tanzania Bara wakati kuna bidhaa kama vocha/kadi ambazo zinafanyia kazi kule Zanzibar; kuna mpango gani wa *TRA* kuyarudisha mapato yale wanayokusanya hapa kwa kadi zile ambazo zinatumiwa kule Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa rufusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la nyongeza lililoulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Cosmas Masolwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo bidhaa nyingine ambazo zinarejeshwa ushuru uliotozwa Bara, ikiwa ni kweli kwamba, tunaweza kutathmini kiasi cha fedha ambacho kinatozwa kwenye simu ambacho kinatumika Visiwani tu. Utaratibu utakuwa ule ule, lakini kwa bidhaa ambazo sasa hivi ushuru wake unaorejeshwa ni zile ambazo unaweza kukokotoa na kwa ushahidi ukaona kwamba, ndio hizi bidhaa zimezalishwa Bara ama zinatumiwa au zinazwa kule Visiwani Zanzibar.

Na. 96

Kuhusu Manufaa ya Bima kwa Vyombo vya Moto

MHE. ZUBEIR ALI MAULID aliuliza:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria vyombo vyote vya moto vinavyoendeshwa barabarani vinatakiwa viwe na angalau bima ya *Third Party*; na kwa kuwa wamiliki wengi wa magari na pikipiki wamekata bima hiyo:-

- (a) Je, ni wakati gani bima hiyo inamnufaisha mwenye chombo kutokana na ajali au matukio mengine ya barabarani?
- (b) Je, ni wakati gani bima hiyo inamsaidia mtu mwingine au mwenye chombo kingine baada ya kugongwa na mwenye chombo chenye bima ya *Third Party*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa rufusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Jimbo la Kwamtipura, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria za Bima za Magari za mwaka 1945 (*Motor Vehicle Third Party Risks Ordinance 1945*) na ya Zanzibar ya Mwaka 1953 (*Motor Vehicle Third Party Risks Decree 1953*), magari yote yanayoendeshwa barabarani yanapaswa kukatiwa bima dhidi ya maumivu ya mwili au kifo kwa wahanga wa ajali barabarani.

Watu wanaolindwa na sheria hiyo ni pamoja na abiria wanaosafiri kwenye magari yaliyoidhinishwa kubeba abiria na wanaolipa nauli au ada iliyokubalika na waendao kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, Bima ya *Third Party* hutoa kinga pia kwa uharibifu wa mali. Bima ya *Third Party* haimsaidii mmiliki wa chombo kilichotakiwa aina hii ya bima, pale anapopata ajali na kusababisha uharibifu wa chombo chake. Mtu anayefaidiwa ni mmiliki wa chombo kilichogongwa na kuharibika.

Hata hivyo, mmiliki wa chombo hicho anatakiwa awe mmiliki halali na bima yenyewe iwe hai wakati wa tukio la ajali. Aidha, dereva wa chombo kilichosababisha ajali lazima athibitishwe na mahakama kuwa ajali hiyo imetokea kwa uzembe wake.

Bima ya Mseto (*Comprehensive Insurance Cover*), ndiyo ambayo inaweza kumfidia aliyesababishiwa ajali na aliyesababisha ajali iliyopelekea kuharibika kwa vyombo husika.

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi sana pamoja na ajali ambazo zimekuwa zikitokea barabarani na vyombo vyote vya moto tunaelewa kwamba kama havina bima hiyo ya *Comprehensive* vitakuwa vinayo hii bima ya *Third Party*, lakini kumekuwa na matukio ambapo madereva au wamiliki wa vyombo hivyo hupatana na wale waathirika wa hizo ajali na kumaliza kulipana kutokea mifukoni. Je, ni lini Serikali sasa itanza kuwaelimisha wananchi kwamba zipo haki za msingi ambazo wanaweza wakalipwa na mashirika ya bima kutokana na ajali wanazozipata kwa kugongwa na vyombo mbalimbali barabarani; pamoja na kuwapunguzia mzigo wamiliki wa magari kwa sababu wanakuwa wameilipia bima hii kihalali?

Mheshimiwa Spika, swali lingine dogo la pili ni kwamba, kumekuwa kukitokea ajali nyingi sana hasa za mabasi humo barabarani na abiria wengi sana wamekuwa wakiathirika pamoja na kupoteza mali zao. Je, ni lini sasa mashirika haya mara zinapotokea hizi ajali na kwenda kuripotwa wataanza kuwafidia abiria ambao wanakuwemo kwenye mabasi haya pamoja na kuwarejeshea sehemu ya mizigo yao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Zubeir Maulid, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuhusu elimu, elimu hii imekuwa ikitolewa na itaendelea kutolewa. Niwapongeze sana wenzetu huko Wizara ya Mambo ya Ndani hasa Polisi, kwa kazi kubwa ambayo wanafanya kuhusu kuwaelimisha wananchi na kusimamia jambo hili. La pili, yule mwenye gari ambaye hafidiwi wakati anapopata ajali, tunategemea kwamba, kama nilivyosema, kama hajakatia chombo chake bima ambayo niliita hapa ya mseto (*Comprehensive Insurance Cover*), basi kwa vyovyote vile kuna uwezekano mkubwa sana kwamba, yeye mwenyewe atakaichukua ile hasara itakayotokana na ile ajali. Vile vile ni kama ile *Third Party* ama ile bima ya mtu wa tatu, tuseme kama haikutosha vilevile kuna njia wazi ya kwenda mahakamani kwa wale ambao watakuwa wameumia. Kwa hiyo, kama kiasi cha bima atakachopata hakitatoshia fidia, basi njia ya pili ni Mahakama yenyewe kutambua na kusema haikutosha na kwa hiyo mnastahili kufidiwa zaidi.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa inanunua magari kwa gharama kubwa; na kwa kuwa magari haya yamekuwa hayawekewi bima; na kwa kuwa magari haya pia yamekuwa yanapata ajali ambazo zinaleta upotevu wa maisha kwa wafanyakazi wa Serikali lakini pia na wale abiria waliosafiri na haya magari; na kwa kuwa haya magari yanakuwa hayana bima wamekuwa wanapoteza haki zao; je, ni sababu ipi ya msingi ambayo inafanya Serikali isiwekee bima magari ambayo yananunuliwa kwa thamani kubwa na kufanya wale watu wanaosafiri kwenye hayo magari wanapoteza maisha na kupoteza haki zao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali haikatii bima vyombo vyake vya usafiri, lakini ijulikane hapa kwamba, Serikali ni kubwa na kwa hiyo tunachukulia kwamba, kama kukitokea madhara yoyote, Serikali ina uwezo wa kufidia pale panapohitajika kufidia. Yule ambaye atakuwa ameumia kutokana na chombo cha Serikali, tunao utaratibu na kama Serikali haikukufidia vya kutosha, basi tuna utaratibu wa Mahakama na tuna kesi nyingi ambazo wale ambao waliumia, walienda mahamani na walilipwa na Serikali. Tuseme kwamba, mara nyingi kwa mfano, ukichukua mali za Serikali hata kupata kampuni au taasisi ya kukata bima ambayo kwa sasa inaweza kuikatia Serikali bima, nafikiri itakuwa haba kidogo kwa sababu ya ukosefu wa mtaji wa kutosha.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), nilikuwa naomba mwongozo wako; katika Kikao cha Sita jana tarehe 4 Novemba, 2008, ziliwasilishwa Mezani taarifa za utendaji kazi wa *TICS* na *TRL*, matarajio ni kwamba,

Wabunge tungepewa taarifa hizo au tungezikuta katika maboksi yetu ya barua, lakini hilo halikufanyika na taarifa hizo zimeandikwa katika vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka mwongozo wako, kwa nini hatujazipata hizo taarifa na zimetoka katika vyombo vya habari?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Said Arfi, kwa sababu nakala ninazo Mezani hapa, wakati wote huu mimi nilikuwa nadhani wenzangu wote huko mmepata nakala za taarifa. Kwa hiyo, hili ni kosa na lirekebishwe ili nakala zipatikane mara moja kutoka Wizara husika na Waheshimiwa Wabunge wapewe. Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yameisha.

Matangazo, kwanza, niongeze orodha ya shughuli za leo ina makosa, Rais Mteule wa Marekani, pamoja na kuwa baba yake anaitwa Hussein Obama, yeye anaitwa Barrack Obama hakuna hilo jina lingine katikati. Kwa hiyo, tumechelewa tu kusaini, ningependa isahihishwe na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wameniidikia kueleza kwamba jina rasmi ni Mheshimiwa Barrack Obama.

Wageni waliopo Bungeni, nitaanza na wageni waliopo kwenye jukwaa langu pale na kwa kuwa wageni hao nadhani hawajui Kiswahili, mniruhusu niwatambulishe kwa Kiingereza.

We have visitors from institutions that are represented here at the Speaker's Gallery and I would ask them to rise when I mention their names. We have M/S Linda Hils from European Commission. She is the Desk Officer for Tanzania in Brussels. We welcome you to Dodoma, welcome to our country and thanks for all that you are doing to coordinate the development activities between the EU and Tanzania. Thanks very much; have a pleasant stay in Tanzania. Amesindikizwa na bwana Theo Caspars, ambaye ni political advisor of the delegation of the European Commission. Theo, is not his first time, we welcome you once again and thanks for your continued support for Parliamentary activities. Yupo pia John Blatio kutoka Ubalizi wa Uingereza, yeye ni mkuu wa The Political Press and Projects, welcome Mr Blatio it is a pleasure to have you once again here in Dodoma. (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa George Lubeleje ni Ndugu Jonas Mwogope, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Mpwapwa, yule pale anatupungia mkono; karibu sana. Wageni wa Mheshiwa Janeth Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum Dar es Salaam ni Ndugu Nuru Daniel, Mwenyekiti wa Mtaa wa Pugu, naona hayupo, Ndugu Yusta Kasamia na Ndugu Imelda Samjela, nadhani hawapo, basi tunaendelea. Wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshiwa Dr. Cyril Chami ni Mheshimiwa Ndugu Louise Mbuya, Diwani kule Moshi Vijijini, karibu sana. Ndugu Aloyce Mlingi ni THEO wa Mji wa Himo, Ndugu Anna Malende ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi na Ndugu Phillip Mtui, Mhandisi wa Halmashauri kule Moshi, karibuni sana. (Makofi)

Wengine ni Viongozi wa Bunge la Chuo cha Ushirika Moshi, ambao ni Ndugu John Safari, ambaye ndiye Spika wa Bunge la Chuo cha Ushirika, karibuni sana na

Ndugu Henry Nico, Naibu Spika. Sasa nyie mngefuata utaratibu wa Bunge hapa, Naibu Spika anatakiwa awe mwanamke au mmojawao lakini karibuni sana. Katibu wa Bunge ni mwanamke, Ndugu Julian Pieson, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, wanaendelea na ziara yao hapa Bungeni. Wale wa Chuo cha Mipango, tunawatakia mafanikio katika mafunzo yenu ili kulijenga Taifa kwa mipango mizuri. Wapo pia wanafunzi 50 kutoka *Club ya United Nations Tanzania Network*, Tawi la Dodoma. Wale 50 wa *United Nations Network*, labda hawakupata nafasi pengine wapo kwenye ukumbi pale chini. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Juma Killimbah ni Waheshimiwa Madiwani Richard Mkumbo, Diwani wa Kinampanda, karibu sana; Mheshimiwa Timothy Kitila, Diwani wa Kata ya Ulemo, karibu sana; Ndugu Michael Abbas, Katibu Kata wa CCM Kata ya Kinampanda; na Ndugu Charles Kiula, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Kyalansangi, karibuni sana. Tunao wanafunzi 35 kutoka Salesian Seminary, pamoja na Walimu wao, karibuni sana. Tunafurahi mnapokuja kujifunza jinsi shughuli zinavyoendeshwa humu Bungeni. (*Makofi*)

Pia tunao wanafunzi 32 wa *School of Nursing* kutoka *St. Johns University Dodoma*, pamoja na Wahadhiri wanne, karibuni sana. Tunawatakia mema, tuna uhaba mkubwa na upungufu wa watumishi katika afya. Tunashukuru sana ninyi mko katika eneo hilo muhimu sana. Wanafunzi 35 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, pengine hawakupata nafasi. Maafisa Waandamizi 15 wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoka Dar es Salaam na wananchi watatu wa Mkoa wa Dodoma, ambao ni Ndugu Grace Kaugira, Ndugu Grace Mahambanyungu na Ndugu Rose Theodos Mgamba. Ahsante sana, huo ndio mwisho wa matangazo ya wageni. (*Makofi*)

Matangazo mengine ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane leo saa saba kamili Ukumbi Namba 219. Mheshimiwa Job Ndugai, ameomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira wakutane leo saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Tangazo la semina; Katibu wa Bunge, anatangaza kwamba, chini ya Mpango wa *Deepening Democracy*, kutakuwa na semina kuhusu *Public Expenditure Review*, ambayo itahusisha Kamati tano; Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati ya Hesabu za Serikali, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Huduma za Jamii, saa saba mchana katika Ukumbi wa African Dream Area D. Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ameiomba nitangaze kwamba, jana Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Kikundi cha Walemavu, ambao wamekuja hapa kwa uzinduzi wa filamu yao inayoitwa Ninge kuwa Rais. Sasa Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa wamekuja kupata msaada wa ufadhili na katika kuwasaidia basi filamu hiyo inauzwa Sh.10,000 kila nakala. Kwa

hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wote, mpate fursa ya kuinunua kanda hiyo, nadhani itapatikana pale yanapouzwa magazeti kwenye eneo letu lile.

Mheshimiwa Ali Ameir, Katibu wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, ameniomba nitangaze kwamba, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, watakutana leo saa tisa na nusu katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Nasikitika kutangaza kwamba, kumekuwa na ajali iliyompata mwenzetu, Mheshimiwa Msambya, leo asubuhi eneo la Gairo. Yeye na wenzake waliokuwa kwenye gari ni wazima na aliweza kupiga simu. Mheshimiwa Mbunge wa Gairo, ametoa msaada, tunapenda kumshukuru sana, amewafikisha hospitali na hali zao zinaendelea vizuri, tuwaombe tu. Kumbe amesharejea, unajua ma-Alhaj hawa wakipata ajali siyo rahisi mambo kuwaendea vibaya. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu, ndugu yangu kila tukisikia mambo ya ajali tunashituka, ahsante sana na pole sana na mshituko ulioupata. (*Makofi/Kicheko*)

Basi hapo ndio mwisho wa matangazo, naomba sasa Katibu atuelekeze katika shughuli inayofuata.

KAULI ZA MAWAZIRI

Wastaafu wa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, Wafanyakazi wa Tanzania waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo ilivunjika tarehe 30 Juni, 1977, waliendeleza ajira zao katika Wizara mbalimbali za Serikali na katika Mashirika ya Umma, yaliyoungwa hapa nchini, kutoa huduma zilizokuwa zinatolewa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile reli, bandari, usafiri wa anga, posta na simu na kadhalika. Kila mfanyakazi aliyestaafu utumishi wake, kwa umri au sababu nyingine zinazokubalika kisheria, alilipwa mafao yake tangu alipoajiriwa katika Jumuiya, yaani *continue service* na huu ni uthibitisho kuwa utumishi wake uliendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Marais wa nchi tatu za iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Tanzania, Kenya na Uganda, walimteua msuluhishi Dr. Obrit, ambaye ripoti yake ilikuwa msingi wa maridhiano, yaani *mediation agreement* ya mwaka 1984. Makubaliano hayo yalikuwa ndio msingi wa mgawanyo wa mali na madeni ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, miongoni mwa madeni hayo ni mafao ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997, baada ya kujitokeza malalamiko kutoka kwa baadhi ya wastaafu wakidai kuwa walipunjwa mafao yao, Serikali iliunda Kamati iliyounganisha wawakilishi wa Serikali na wale wa wastaafu hao, wakiongozwa na Bwana Musoka na Kaguga Biengo.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo iliwezesha na Serikali na ilitembelea Kenya na Uganda, kupata uzoefu wa jinsi nchi hizo zilivyoshughulikia mafao ya wastaafu hao.

Ripoti ya Kamati hiyo, pamoja na mapendekezo yake yaliwasilishwa Serikalini na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999, Serikali ilianza kulipa mafao ya wastaafu hao kulingana na mapendekezo ya Kamati hiyo iliyoundwa mwaka 1997. Wastaafu wote wa Jumuiya waliostahili kulipwa walilipwa malipo yaliyojumuisha riba ya malimbikizo ya asilimia saba, kwa mujibu wa kumbukumbu za kila mmoja wao, ambazo zilithibitishwa na Mashirika yaliyorithi ajira zao. Baada ya kulipwa, wastaafu hao walianza kulalamika kwamba, walipunjwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 wastaafu hao walifungua kesi Mahakama Kuu ya Tanzania, kesi namba 95 ya mwaka 2003, wakidai walipwe mafao ambayo waliamini walistahili zaidi ya yale waliyokuwa wamelipwa. Mwaka 2004, Serikali iliteua Kamati nyingine ya muafaka, iliyohusisha Wawakilishi wa Serikali na wastaafu hao, kuangalia upya madai yao na kufikia muafaka wa jinsi ya kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, majadiliano kati ya Wawakilishi wa Serikali na wale wastaafu yaliendelea na mapendekezo ya Kamati hiyo yalifikishwa katika Baraza la Mawaziri mwezi Juni, 2005. Baraza lilipitisha uamuzi kwamba, wastaafu hao walipwe kwa utaratibu uliopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, majadiliano hayo kati ya Wawakilishi wa Serikali na wale wa Wastaafu, hatimaye yalizia Hati ya Makubaliano, yaani *Deed of settlement* ya tarehe 20 Septemba, 2005, ambayo ilisainiwa na wawakilishi wa pande zote mbili. Hati hiyo ya makubaliano ilifikishwa Mahakama Kuu na kupewa haki ya hukumu na Mahakama ya kuthibitisha madai ya wastaafu hao na Serikali. Hukumu hiyo ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Jaji Urjo, ilitamka kama ifuatavyo na ninaomba kunukuu: *“The suit is hereby marked settled.”*

Mheshimiwa Spika, hati ya makubaliano ilibainisha wazi mambo yafuatayo:-

Moja, wastaafu wa iliyokuwa *East African Community* walikubali kufuta madai yao yote yaliyokuwa katika kesi namba 95 ya mwaka 2003.

Pili, Serikali ilikubali kuwalipa wadau wote waliofungua kesi Mahakamani na wengine wote waliofanya kazi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla ya Juni 30, 1977 na baada ya malipo hayo Serikali haingedaiwa tena.

Tatu, Serikali ilikubali kuwalipa wadai 31,831 jumla ya shilingi 117 bilioni, kwa misingi ya stahili ya kila mmoja kulingana na taarifa ya kila mmoja kwenye jalada au nyaraka nyingine zilizothibitishwa. Aidha, Serikali ilikubali kuchukua gharama za Mawakili wa wadai ili malipo wanayolipwa wastaafu hao yasikatwe chochote.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hati hiyo ya makubaliano, hadi tarehe 30 Septemba, 2008, Serikali ilikuwa imewalipa wastaafu 31,444 na imetumia takriban shilingi bilioni 114.2 kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 20.

Wafanyakazi waliokuwa *Cargo* walikuwa 7,521, walilipwa zaidi ya shilingi 23,181,404,216.68. Wafanyakazi wa iliyokuwa Bandari walikuwa 3,588, walilipwa jumla ya shilingi 1,277,461,661.90. Wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Reli walikuwa 11,326, walilipwa jumla ya shilingi 38,669,967,032.3. Wafanyakazi wa iliyokuwa *TTCL* walikuwa 2,901 na walilipwa jumla ya shilingi 106,725,000,755.58. Wafanyakazi wa Posta walikuwa 1,041 na walilipwa jumla ya shilingi 4,300,384,376.11. Wafanyakazi wa Benki ya Posta walikuwa 25 na walilipwa jumla ya shilingi 89,883,931.85. Wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Ndege walikuwa 1,028 na walilipwa jumla ya shilingi 8,934,212,878.39. Wafanyakazi waliokuwa kwenye Mfuko Mkuu, yaani Makao Makuu ya Jumuiya walikuwa 4,014 na walilipwa jumla ya kiasi cha shilingi 15,607,110,143.11.

Kwa ujumla wafanyakazi au wastaafu ambao wameshalipwa walikuwa 31,444 na walilipwa jumla ya shilingi 114,229,588,395.93.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kulipa bado linaendelea kwa wale wanaoleta uthibitisho kwamba hawakulipwa na walikuwa watumishi halali wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanastahili kulipwa. Wapo wengine ambao walipunjwa mafao yao katika ukokotoaji nao ikithibitika hivyo wanalipwa. Ili kuepuka udanganyifu, tunashughulikia wadai mmoja mmoja na siyo vikundi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kukokotoa mafao ya wastaafu hawa, vigezo vilivyozingatiwa na vinavyoendelea kuzingatiwa ni hivi vifuatavyo:-

Moja, Sheria za Pensheni na Kiinua Mgongo za iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mbili, Sheria na Kanuni za Fedha.

Tatu, Maridhiano (*Mediation Agreement*) ya Mwaka 1984.

Nne, Sheria Namba 2 ya Mwaka 1987.

Tano, Hati ya Makubaliano ya tarehe 20 Septemba, 2005 (*Deed of Settlement*).

Sita, hukumu ya Mahakama Kuu ya tarehe 21 Septemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, karatasi zitakazogawanywa pale imeandikwa 21 Februari, nitaomba Waheshimiwa Wabunge, wafute Februari na waweke Septemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la kuwalipa wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, matatizo mbalimbali yalijitokeza kama ifuatavyo:-

- (a) Upungufu wa nyaraka ambazo zimechelewesha zoezi hili kuweza kukamilika mapema zaidi.
- (b) Madai yasiyo na ushahidi au ushahidi wa maneno.

(c) Madai ya wafanyakazi wasiohusika kabisa wala kustahili malipo yoyote kama vile walioajiriwa baada ya kuvunjika kwa Jumuiya tarehe 30 Juni, 1977; waliostaafu kabla ya Jumuiya kuvunjika; waliokuwa vibarua wa iliyokuwa *Cargo*; wafanyakazi wa iliyokuwa *Bora Shoes*; wafanyakazi wa iliyokuwa *East African Breweries*; na wafanyakazi wa iliyokuwa UDA au KAMATA.

(d) Wafanyakazi wa Taasisi zilizoondolewa kwenye Jumuiya kabla ya Jumuiya kuvunjika kama vile Watumishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine na Watumishi wa Idara ya Kodi ya Mapato.

Pamoja na matatizo hayo, Wizara yangu imeendelea wakati wote, kuyashughulikia matatizo mengine au masuala yoyote yanayowahusu au kuwagusa Wastaafu hawa kila yalipowasilishwa Wizarani, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, wanatendewa haki kwa mujibu wa hati ya makubaliano ya Mahakama Kuu.

Kuibuka kwa makundi mbalimbali kutaka kulipwa mafao wakidai yapo malipo ya Serikali ya Awamu ya Nne. Tatizo hili linatokana na uelewa wao kuwa fedha walizolipwa zilikuwa kwa ajili ya ahadi ya Serikali ya Awamu ya Tatu na kwamba, yapo malipo mengine yatakayolipwa na Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kile wanachokiita malipo halisi kwa imani yao kuwa yapo mabilioni ya fedha kwa pesa za Uingereza yaliyoletwa na Malkia wa Uingereza.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na uelewa wao huo, mapema mwaka huu lipo kundi la Wastaafu waliowasilisha ombi Mahakama Kuu, wakiomba Mahakama itoe tafsiri ya neno thamani halisi, yaani *real value*. Pamoja na kwamba, Mahakama haijatoa uamuzi wa kesi yao, kundi hilo limekuwa likiandamana na kujikusanya mbele ya lango kuu la Ikulu, Ofisi za Wizara ya Fedha na Uchumi na katika viwanja vya Ukumbi wa Karimjee na hivi karibuni walitanda barabarani eneo la Daraja la *Salander* na kuzuia magari yasipite.

Matukio hayo yamefanywa kwa nyakati tofauti ili kuishinikiza Serikali iwalipe fedha inayotokana na kile wanachokiita thamani halisi. Aidha, pamoja na jitihada za Viongozi mbalimbali wa Ikulu na Wizara ya Fedha na Uchumi, kufanya vikao na wastaafu hao, wamekuwa wakishinikiza wote walipwe bila kufanyiwa uhakiki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na madai mengine mengi, Viongozi wachache wa kundi hilo wanapita kila mahali hapa nchini, wakikusanya michango inayodaiwa kusukuma madai ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki dhidi ya Serikali. Haya yote ni udanganyifu na upotoshaji wa makusudi, wenye lengo la kutoa matumaini kwa wastaafu ili wajipatie mapato yasiyo halali kutoka kwa wastaafu hao.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya maeneo mawili ya hoja zinazotumiwa vibaya na baadhi ya Wastaafu wanaojifanya kuwa Viongozi wa wenzao, ambao kwa hakika wanatumia nafasi hiyo, kuwadanganya na kuwapotosha Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kujinufaisha. Hoja zao ni kwamba:-

(a) Kuna kiasi cha fedha zilizopokelewa na Serikali kutoka kwa *Crown Agency* ya Uingereza.

(b) Kiasi cha fedha hizo zilizopokelewa za kigeni ni jumla ya shilingi bilioni 450 na siyo shilingi bilioni 117 zilizoidhinishwa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2008, Wizara ya Fedha na Uchumi, iliendesha zoezi maalum la kuwasihi wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwasilisha madai yao mmoja mmoja ili yaweze kuchambuliwa na kuhakikiwa. Zoezi hilo lilifanyika kutokana na swali aliloulizwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni na ambaye aliigiza Wizara ya Fedha ifanye uhakiki. Baada ya uhakiki, Wastaafu 4,289 walikubali kufuata utaratibu huo.

Uhakiki ulionyesha kuwa, waliostahili kulipwa ni Wastaafu 21 tu na stahili hiyo ni mapunjo yaliyotokana na dosari katika ukokotoaji wa hesabu. Madai ya Wastaafu 194 yalionyesha kuwa walikuwa vibarua na hivyo hawakustahili kulipwa mafao yoyote. Wastaafu 474 walikwisha lipwa mafao yao yote kwa mujibu wa hati ya makubaliano ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana nao kuwa, Sheria ya *East African Community Mediation* ya 1987 na Barua ya *Crown Agency* ya kuwasilisha fedha za Mafao ya Watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, vyote vinabainisha kwamba Serikali ya Tanzania ilipokea kutoka kwa msuluhishi, *Pound* za Uingereza 9,189,410.54, sawa na *Dollar* za Marekani 13,793,305.01, wakati huo *Pound* ya Uingereza ilikuwa sawa na *Dollar* 1.50099 mwezi Juni, 1987. Kiasi hicho kilikuwa sawa na shilingi za Kitanzania 114,697,125.60.

Napenda kurudia kwamba, thamani ya *Pound million* 9 zilizopokelewa na Serikali kwa wakati huo; Juni, 1987, zilikuwa ni sawa na shilingi za Kitanzania 114,697,125.60, wakati huo *Dollar* moja ya Uingereza ilikuwa ni sawa na shilingi 8.31 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Dr. Umbrich, mgao wa mafao baada ya Jumuiya kuvunjika ulikuwa ni *Pound* za Uingereza 2,915,592.36 na *Crown Agency* walikuwa Wakala wa kuwekeza fedha hizo na hivyo mgao wa mafao ya wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa kama ifuatavyo: Kenya walipata mgao wa *Pound* 19,755,337.79; Tanzania ilipata mgao kama nilivyosema wa *Pound* 9,189,410.54 na Uganda walipata mgao wa *Pound* 70,844.03.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ya Tanzania ilipokea kiasi cha *Pound* za Uingereza 9,189,410.54 kutoka *Crown Agency*, tarehe 20 Januari, 1987, kwa ajili ya *pension* na kiinua mgongo kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Fedha hizo zilifika Benki Kuu ya Tanzania kupitia Benki Kuu ya Uingereza, yaani *Bank of England* wakati huo, mwaka 1987, zilikuwa kama nilivyosema shilingi 114,697,125.60. Fedha hizo ilipofika mwaka 2005 zilikuwa sawa na shilingi za

Kitanzania 2,468,868,189,617.84 baada ya kuwekewa riba ya 17.53% kwa vile zilikuwa zimewekezwa katika dhamana ya Serikali, yaani *Government Stock Average Rate* kwa muda wa miaka 19; yaani 1987 – 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, stahili sahihi ya wastaafu hawa kama ilivyoelezwa, ingekuwa shilingi 2,468,000,000,000, Serikali baada ya kuzingatia mambo mengi ya kibinadamu, iliamua kuwalipa wastaafu hawa jumla ya Shilingi 117 bilioni, kiasi ambacho ni zaidi ya shilingi 114.5 bilioni za walipa kodi, ukilinganisha na kiasi cha fedha walichostahili kulipwa.

Kiasi cha fedha walicholipwa ndicho kilichoamuliwa na Mahakama, kwa kuzingatia hati na makubaliano ya kesi namba 95 ya 21 Septemba, 2005 na siyo shilingi bilioni 450 walizodai walipwe.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha madai kilifikiwa na wastaafu kwa kuchukua mafao yaliyopaswa kulipwa mwaka 1977, kwa shilingi ya Tanzania na kuyabadilisha katika *Dollar* ya Marekani kwa kiwango cha ubadilishaji cha shilingi 8.31 kwa *dollar* moja mwaka 1977. Baada ya kuyabadili mafao hayo katika *dollar* ya Marekeni, wastaafu waliongeza riba ya malimbikizo ya 7% hadi Machi, 2005, hatimaye dola hizo walizibadilisha tena kuwa shilingi ya Tanzania kwa thamani ya mwaka 2005 ya shilingi 1,100 kwa *dollar* moja, ndiyo wakafikia madai yao ya shilingi bilioni 450.

Mheshimiwa Spika, kigezo hicho kilichotumiwa na wadai kilikataliwa kwa sababu kwa mujibu wa Sheria za nchi, fedha inayotumika Tanzania kwa malipo halali ni shilingi ya Tanzania na fedha iliyopokelewa kutoka *Crown Agency* ilikuwa imewekezwa katika Shilingi ya Tanzania.

Ili kukidhi matakwa ya wastaafu, Serikali ilitumia wastani wa riba ya dhamana za Serikal, yaani *Average Government Stock Rate* ya kipindi cha mwaka 1987 – 2005, ambayo ni 17.53%, kwa lengo la kulinda thamani ya mafao yao.

Utaratibu wa kuwalipa wastaafu hao mafao yao pamoja na riba, ulichukuliwa kuwa ni maalum, kutokana na mazingira ya madai yao kwa sababu hakuna Sheria ya Pensheni yoyote hapa nchini, yenye kipengele cha kumlipa mstaafu mafao na riba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, Serikali inatoa tamko kama ifuatavyo:-

(a) Malipo ya Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, yamefanyika kwa misingi ya haki na Sheria kwani yamezingatia Hati ya makubaliano iliyohitimishwa na Mahakama, Kanuni na Taratibu za nchi. Kwa hiyo, hakuna malipo mengine nje ya Hati ya Makubaliano ya Mahakama Kuu na Serikali inapenda kuwashauri wananchi wasidanganywe.

(b) Kutokana na matatizo yanayoweza kujitokeza kwa mtu mmoja mmoja, kama ilivyojitokeza katika zoezi la mwezi Septemba, 2008, Wizara yangu itaendelea kupokea maombi ya aina hiyo kutoka kwa wastaafu halali na kuyashughulikia ipasavyo.

(c) Kwa mfano, kati ya wastaafu 21 halali niliowataja hapo awali, waliodhihirika kuwa wanastahili kulipwa ni wastaafu kumi, ambao hundi zao zipo tayari na wanaweza kuzichukua wakati wowote pale Makao Makuu ya Wizara Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nimetoa ufafanuzi huu kwa kirefu hapa Bungeni, kwa lengo la kulifahamisha Bunge lako Tukufu, hali halisi ilivyo kuhusu madai ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla, kulielewa kwa kina suala hili. Aidha, Serikali inatoa wito kwa wastaafu wote wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kukubali kuwa, malipo yaliyokwisha kulipwa baada ya uhakiki na baada ya kuidhinishwa na Mahakama Kuu ya Tanzania ni halali kufuatana na Hati ya Makubaliano ya Mahakama Kuu.

Vilevile, Serikali inawasihi sana wazee hawa, wajiepushe na upotoshaji na udanganyifu wa wajanja wachache, wanaojinufaisha kupitia migongoni mwao kwa visingizio vya kuendelea kusimamia madai ambayo kwa kweli hayapo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kabla sijamwita Katibu kwa shughuli inayofuata, naomba radhi nilikosea, ile semina ya *Public Expenditure Review* ni kesho saa saba mchana, yaani Alhamisi tarehe 06 Novemba, 2008.

Kwa hiyo, naomba wenzetu ambao hawapo, waweze kufahamu hivyo kwamba ni kesho saa saba katika Ukumbi wa African Dream kule Area D ya Kamati za Fedha na Uchumi, Hesabu za Serikali, Hesabu za Mashirika ya Umma, Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Huduma za Jamii. Katibu kwa shughuli inayofuata.

**UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI YA CHUO KIKUU HURIA CHA
TANZANIA
NA BARAZA LA CHUO KIKUU CHA
SAYANSI ZA AFYA MUHIMBILI**

SPIKA: Nitamwita sasa msimamizi wa uchaguzi, *Returning Officer* wetu ili atoe maelezo kuhusu chaguzi hizo mbili. Katibu.

DR. THOMAS D. KASHILILAH – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia Siku ya Jumamosi, tarehe 01 Novemba, 2008 na Jumatatu tarehe 03 Novemba, 2008, leo tarehe 05 Novemba, 2008, baada ya kipindi hiki cha maswali kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge wanaoliwakilisha Bunge katika Mabaraza ya Vyuho Vikuu vifuatavyo; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa mwisho wa kurudisha *form* za kuomba uteuzi ilikuwa ni Jumatatu tarehe 03 Novemba, 2008 saa kumi jioni. Muda huo ulipofika, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamejitokeza kuchukua na kurejesha *form* walikuwa watano kama ifuatavyo: Nafasi tatu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo na Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame.

Hata hivyo, asubuhi hii tumepokea taarifa rasmi kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, akiomba kuondoa jina lake, hii ikiwa inaonyesha kwamba sasa wagombea waliobaki ni watatu ambao ndiyo wanaotakiwa kwa mujibu wa taratibu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nafasi moja katika Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili, aliyerejesha *form* ni mmoja na anayetakiwa ni mmoja ambaye ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. (*Makofi*)

Ni vyema tuelewe kwamba, uchaguzi huu unaendeshwa kufuatana na masharti ya Kanuni ya 12 na nyongeza ya pili ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, ambazo zinafafanua taratibu zinazotakiwa katika kufanya chaguzi katika Vyuo na Bodi mbalimbali.

Hata hivyo, kwa taratibu na mazoea yaliyojitokeza katika taratibu zilizopita, wagombea wanaopita bila kupingwa huwa wanapigiwa kura ya NDIYO moja kwa moja, kwa kauli moja, badala ya kujaza nakala za karatasi ya kura.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa niombe Bunge lako lifanye uamuzi kupiga kura ya moja kwa moja au kutumia mazoea kwa kuwapigia kura ya kauli ya NDIYO kwa wagombea wote.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana Kaimu Katibu wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge, sidhani kama tunahitaji kuhojiwa hapa kuhusu hili, kwa sababu imekuwa ndiyo utaratibu tunapokuwa na jina moja kwa nafasi moja au majina mawili kwa nafasi mbili au majina matatu kwa nafasi tatu, kwa maana nyingine kunakuwa na uchaguzi usiokuwa na ushindani. Kwa hiyo, sioni kama ni vyema kuwahoji ila sasa nitamwomba Katibu atamke kwenye kila nafasi halafu mtajibu tu kwa sauti ya ujumla.

KAIMU KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, katika nafasi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, mgombea wa kwanza ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, mgombea wa pili ni Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya na mgombea wa tatu ni Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa wagombea hawa wote tunaafiki?

WABUNGE: Ndiyo,

SPIKA: Basi wamepita hao. (*Makofi*)

KAIMU KATIBU WA BUNGE: Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya Muhimbili, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. (*Makofi*)

SPIKA: Asimame tafadhali. Kwa huyo naye Waheshimiwa Wabunge tunaafiki?

WABUNGE: Ndiyo.

SPIKA: Ahsante sana, shughuli ya uchaguzi imekwisha sasa nitatoa kama kawaida, nafasi fupi dakika zisizozidi tatu, kwa waliochaguliwa kuweza kushukuru. Nitaanza na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, karibu tafadhali.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, mimi nashukuru sana kwa sababu siku hii ni ya kihistoria kwamba, taifa kubwa kabisa limemchagua mtu mwenye asili ya Kiafrika, hasa kutoka sehemu zetu za Afrika Mashariki kuwaa Rais wa nchi hiyo. Labda kwa kufuatia mtiririko huo na sisi hivi leo tumechaguliwa bila kupingwa, kuliwakilisha Bunge letu Tukufu katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nashukuru sana na tutaendelea kuliwakilisha Bunge letu kwa ufanisi kama tulivyokuwa tukifanya huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine, nawashukuru tena, mlinipa nafasi hii katika kipindi kilichopita, ambapo nilikuta Baraza muda wake umebakia mwaka mmoja tu kumalizika. Ninashukuru tena kwamba, mmenipa imani hiyo kwa mara ya pili, naahidi nitafanya kama ambavyo inatakiwa. Kimoja tu, kwa kukaa kwa ule muda wa mwaka mmoja kwenye lile Baraza, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tupo wengi ambao tayari tumejisajili, lakini nawaomba na wengine tuendeleo kujisajili, fursa nyingi zipo tunahitaji wasomi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wetu na maendeleo ya Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Mheshimiwa Benson Mpesya, karibu tafadhali.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba nisimame kwa unyenyekevu mkubwa, kuwashukuru Wabunge wenzangu, kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mwakilishi wa Bunge katika Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ninaomba niwahidi kabisa kwamba, nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu wote na kadiri atakavyonijalia Mwenyezi Mungu, kuhakikisha ninawawakilisha kikamilifu.

Naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa kufanya safari yetu ya kugombea iwe nyepesi zaidi. Tunamshukuru sana kwa uamuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Karibu.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa, nachukua nafasi hii, kwanza kabisa, kukushukuru wewe na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha, ninaahidi kwamba, nitaliwakilisha Bunge lako Tukufu kwa itifaki zote na nitakuwa kiungo kati ya Bunge na Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili.

Kwa hayo machache, ninasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, kabla hatujamaliza hatua hii, nilipenda nisisitize jambo moja kwenu; Waheshimiwa Wabunge, kitendo cha Dr. Lucas Siyame, mtaona kwamba hata kilichotokea kwa maana ya uwakilishi, tuna mjumbe mmoja ambaye ni Mbunge kutoka Upinzani, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kuzingatia jinsia. Sasa ushindani ulikuwa unabaki baina ya Mheshimiwa Mpesya na Mheshimiwa Siyame. Wote wawili wanatoka Mkoa wa Mbeya na ushindani wa namna hii huwa unaleta kidogo utata.

Sasa mwenzetu huyu mmoja akaona ni vizuri amwachie mwenzie, hili ni jambo ambalo lazima tuisitize. Kwa sababu hakuona uhalali wa kuendelea kupimana nguvu, kuendesha kampeni na hivi akasema inatoshwa tunatoka mkoa mmoja tusijenge ufa. Nakupongeza sana Dr. Siyame kwa hatua yako hiyo ya kiungwana. *(Makofi)*

**AZIMIO LA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUMPONGEZA RAIS MTEULE WA MAREKANI,
MHESHIMIWA BARRACK OBAMA**

MHE. WILSON M. MASILINGI – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa heshima nawasislisha taarifa kwamba, katika Kikao cha Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kilichokaa kuanzia saa 4.00 mpaka 4.30 asubuhi, tumetafakari Agizo la Bunge Kuandaa Azimio la Kumpongeza Rais Mteule wa Taifa la Marekani, Mheshimiwa Barrack Obama na tumekamilisha kazi yetu. Kwa heshima kubwa, nawasilisha mapendekezo ya Azimio hilo liweze kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

KWA KUWA, leo Jumatano tarehe 05 Novemba, 2008 Mheshimiwa Barrack Obama ametangazwa kuwa Rais Mteule wa 44 wa Marekani (USA) kupitia Chama cha *Democrat*;

NA KWA KUWA, kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Barack Obama kuwa Rais Mteule wa Kwanza mwenye asili ya Kiafrika ni ushahidi wa kukomaa kwa demokrasia nchini Marekani; (*Makofi*)

KWA HIYO BASI, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linampongeza Mheshimiwa Barack Obama kuwa Rais Mteule wa 44 wa Marekani na pia linawapongeza wananchi wote wa Marekani kwa utulivu na amani wakati wa mchakato wa uchaguzi; na kwa kuonyesha uwezo wao wa kuleta mabadiliko katika Siasa za Marekani kwa kumchagua Mheshimiwa Barack Obama kuwa Rais wao. (*Makofi*)

VILEVILE, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linampongeza Mheshimiwa Joe Biden, Mgombea mwenza kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais Mteule wa Marekani;

AIDHA, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linampongeza mgombea kupitia Chama cha *Republican*, Mheshimiwa John McCain kwa kuonyesha uungwana na ukomavu wa kisiasa katika hotuba yake ya kukubali matokeo ya kura na kuwaomba Wamarekani wote waungane nae kumpa ushirikiano Rais Mteule Mheshimiwa Barack Obama. Tunampongeza sana kwa uungwana huo wa kistaarabu

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa hoja hiyo, inayojieleza yenyewe. Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono na nimepata maombi ya wenzetu wanne ambao wanataka kuichangia kidogo kuirutubisha, nao ni Mheshimiwa Khalifa, Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

Nitamwita sasa Mheshimiwa Khalifa kwa dakika chache halafu ataendelea Mzee Malecela.

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii, katika siku hii muhimu sana katika historia ya dunia na Bara zima la Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sisi Kambi ya Upinzani ambao mimi nazungumza natokea upande huo, tumefurahishwa sana na kitendo hiki walichokifanya wenzetu wa Marekani, kwa kuonyesha kuwa misugvano ya kijamii ambayo imekuwepo kwa muda mrefu katika historia ya Taifa hilo sasa imeanza kumalizika.

Hali hii sio tu itasaidia katika kuwaunganisha Wamarekani lakini pia itasaidia katika kutoa sura kwa sehemu nyingine za ulimwengu, kwa sababu Marekani ni Taifa

kubwa. Kwa muda mrefu wenzetu wa Marekani wamekuwa mbele katika kuhimiza demokrasia na haki za binadamu duniani, lakini mimi nina hakika kuwa kitendo walichokifanya kitawaongezea nguvu katika harakati zao hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema tu kwa hili walilolifanya wenzetu ni funzo, tena funzo zuri kwa vile sisi wengine tunapaswa kulitumia funzo hili katika nchi zetu na katika dunia yetu. Kwa sababu kimsingi, sote tunaomba uongozi ili tuwaongoze wenzetu, tuwaunganishe wenzetu, kwa faida yao na kwa faida ya Mataifa yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, nabadili mpangilio kidogo ili Mheshimiwa Malecela aje mwisho atufungie dimba hili kwa hadhi yake. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo halafu ndio Mheshimiwa John Cheyo na hatimaye Mzee wetu Mheshimiwa John Malecela.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi naona faraja sana, kupewa nafasi hii adimu, kupongeza na kuunga mkono Azimio ambalo limesomwa kwa tukio kubwa la kihistoria katika dunia yetu hii ya leo. *(Makofi)*

Mimi binafsi na kwa niaba nadhani ya Watanzania wengi wanaonisikiliza, nasema na mimi nampongeza sana Mheshimiwa Barrack Obama. Wengine tulifuatilia kwa muda mrefu tukisema bwana mdogo, lakini nadhani ametoa chachu kwamba sasa mtazamo umebadilika. Mtazamo umebadilika kwa maana kwamba, watu hawaangalii tena. Zamani tulikuwa tunaona kwamba, kiongozi ni lazima awe mtu labda wa makamo Fulani, lakini kumbe ni uwezo na sera za chama ambacho anatoka kwa maslahi ya watu ambao atawaongoza. Binafsi naomba nilipongeze sana hilo jambo, lakini vilevile nadhani ni fursa kubwa sana ya kuwapongeza Wamarekani. Kama mwenzangu alivyokwishasema, wameonyesha demokrasia ipo, wengi tulikuwa na wasiwasi hadi jana tukaona hali ya hewa inabadilika lakini kumbe basi demokrasia ya kweli ipo, inawezekana kila mahali, Marekani imewezekana na kwingineko inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nikipongeze sana chama chake cha *Democrat*, kwa sera zake ambazo zimeonekana kuaminika na kukubalika kwa wengi walioko Marekani na hata kumpa ushindi huo, lakini yeye mwenyewe pia akiweza kuzitetea na kuzisimamia.

Kama mwanamama, nitakuwa mnyimi wa fadhila, nisipompongeza mke wake. Mke wake amefanya kazi kubwa, tuliokuwa tunafuatilia tumeona kwa ari kubwa amejitoa, pamoja pengine na nafasi kuwa kubwa mno, lakini aliweza kuonyesha umahiri wake. Hata pale unapona wanasema kila mwanamume unapona anafanikiwa, basi jua kuna mwanamke mwenye nguvu nyuma yake anahangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla, nadhani ni vyema kabisa tukampongeza Mama Hillary Clinton. Huyu ameonyesha

mfano wa ajabu, pamoja na kushindwa lakini aliweza kuonyesha mshikamano na ushirikiano wa ajabu kwa kutetea sera za chama chake na maslahi ya Marekani kwa ujumla. Ndugu zangu ni mfano wa kuigwa, hata kama ambapo tunashindwa, tuendeleo kusimama na misimamo yetu. Kikubwa nadhani sisi Watanzania tumejifunza kwamba, kuangalia ni nini tunataka yale mengine madogo madogo yataangaliwa kwa wakati wake, lakini tuangalie ni sera gani kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu na vyama vyetu. Kwa hiyo, nadhani tunaposhindwa tukubali kushindwa na tunaposhinda pia tukubali kushinda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme binafsi nimeona nisimame niunge mkono hoja hii, nikiwapongeza sana Watanzania. Tulikuwa tunazungumza kila kona kwa muda mwezi mzima, laiti na chaguzi zetu zingekuwa namna hii. Kila mtu alikuwa anafuatilia mpaka Kilindi walikuwa wanafuatilia. Kwa hiyo, tumeonyesha mfano na mshikamano na hata wenzetu nadhani mwakilishi wa Marekani wa Siasa, ambaye yupo hapa, tuliopata fursa kuzungumza naye ameona jinsi Watanzania tunavyoathamini Taifa lao, lakini pia tunauthamini utu, demokrasia ya kweli na ubinadamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sana nirejee tena kusema katika yote hayo, naomba sana tumtangulize Mwenyezi Mungu. Marekani wamefanya hivyo, tulikuwa tunashirikiana sala mbalimbali kwenye *website* zote, madhehebu yote bila kujali ni dini gain, lakini yamewezekana. Ninaomba sana Mungu na sisi Watanzania sasa kwa yale mema ambayo yametendeka, basi kuanzia leo kwa sababu tumefuatilia kwa makini basi tuendeleo kuyafuatilia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nasema tena pongezi. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nataka kuungana na wenzangu, kuwapongeza Wananchi wa Amerika, kwa kutoa uamuzi wao kwa hali ya utulivu, pamoja na mvua, lakini kulikuwa na watu wengi sana ambao walikuwa wamevumilia na kuweza kutimiza haki yao ya kuchagua. Pia nampongeza sana ndugu yetu hapa hapa Kenya, kwa kuzaliwa Mheshimiwa Barrack Obama, kwa sababu hii ndio inaonyesha kwamba sisi tupo kila mahali, siwezi kusema mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kikubwa natumaini Watanzania tujifunze kitu fulani kutoka kwa Waamerika na zaidi kutoka kwa Rais Mteule Barrack Obama. Barrack Obama katika mazungumzo yake yote, kwa mara ya kwanza amesisitiza Uamerika, Taifa kupendana, kuacha mambo yanayotutenganisha. Hakuna rangi, dini, sisi wote ni Waamerika na kama ulisikia *speech* yake leo asubuhi, ilikuwa ni jambo hilo hilo. Sasa kama Taifa kubwa kama Amerika, linaweza likaona kuna umuhimu wa kujali Utaifa, je, vipi Taifa dogo kama letu; tuisitize jambo hili la Utaifa? (*Makofi*)

Ni vizuri sote tukakaa tukajiuliza tunafanya nini kujenga kama Tanzania; pamoja na kwamba Tanzania ni kubwa zaidi ya vyama vyetu; ni kubwa zaidi ya dini zetu; Tanzania ndio kimbilio la watoto na vizazi vyetu vijavyo. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana tunapofanya mambo yetu hata tunapozungumza kwenye siasa, hata tunapofuatilia

mambo ambayo labda Serikali imekosea au mtu mwingine amekosea, tujue ni kiasi gani tunaumiza au tunajenga Tanzania. Mimi naona hili ndilo jambo kubwa la kujifunza na Obama ameonyesha mtu mwenye asili ya Afrika anajali nchi yake. Mimi naona tufuate hayo ya Obama na ninatumaini hili litakuwa ni somo kubwa sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais Mteule na Watanzania nawaomba tuipe ambayo tumeyaona. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa kuhitimisha sasa Mheshimiwa John Samwel Malecela.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa heshima kubwa ya kuhitimisha Azimio hili ambalo kama Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje, nilikuwa mmojawapo wa wale ambao walipewa shughuli ya kutayarisha Azimio hili.

Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Mteule, ndugu yetu Barrack Obama, kwa kuchaguliwa na kuja kuitawala nchi ya Marekani. Mimi nilipata bahati na ninasema kwa unyenyekevu mkubwa, kuishi karibu miaka mitano Marekani. Katika miaka hiyo ya nyuma, tukichukua historia ya Marekani tukumbuke kwamba, hii ndiyo nchi ambayo ilikuwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe, iliyotokana na hisia za rangi kwamba wengine walitaka weusi wawe hivi, wengine walitaka vinginevyo na wakawa na vita ya wenyewe kwa wenyewe, lakini ushindi ukaenda kwa wale wenye mawazo pevu ya kusema Marekani ni nchi moja na iwe ya Wamarekani wote.

Mimi pia nataka nikipongeze chama chake cha *Democratic* kwamba, kilimteua na ni kweli baada ya kuteuliwa kwake, tumeona jinsi chama chake kilivyomfanyia kazi. Watu walipita mlango kwa mlango, nyumba kwa nyumba, bila ya kujali ikafika hata mtu kwa mtu. Sasa haya ni mambo ambayo tunahitaji kujifunza. Lngine kubwa ambalo tujifunze ni la Utaifa na mimi nataka nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kwamba, Baba wa Taifa, ametuachia nchi yenye amani na utulivu sasa ni wajibu wetu kuona kwamba, utulivu huu katika Tanzania unaendelea. Vilevile swali letu daima lisiwe Serikali ya Tanzania inanifanyia nini ila wewe kama Mtanzania, unaifanyia nini Serikali yako. (*Makofi*)

Tunampongeza sana Barrack Obama, ambaye ameteuliwa lakini tunajua na tunamwomba sana, kazi yake kubwa anaongoza Taifa kubwa lenye nguvu kuliko Mataifa yote duniani. Kwa hiyo, atabeba mzigo mkubwa wa kuhakikisha kwamba, amani ipo duniani, yaani amani inakuwa kila mahali. Tunajua kwamba, changamoto atakayokuwa nayo ni kubwa sana na ndiyo sababu ninakubaliana na wale wote wanaosema tuendelee kumwomba ili Mwenyezi Mungu ampe nguvu, uwezo wa kuubeba mzigo huo mkubwa sana.

Kwa sisi wa Tanzania na wa Bara la Afrika, tunampongeza sana kwamba, kwa mara ya kwanza katika historia ya dunia, mtu mwenye asili ya Uafrika anatawala kwenye dola ambalo ni kubwa na lenye nguvu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba niwapongeze pia Ubalizi wa Marekani, ambao wapo hapa. Sasa waendeele kujenga uhusiano mzuri, ambao utakuwa wa karibu zaidi na Tanzania hasa kutokana na kitendo hiki ambacho kitajenga uhusiano mzuri kati ya Afrika na Taifa kubwa la Wamarekani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hakuna haja yoyote ya kumwita mtoa hoja, kwa sababu Azimio limeungwa mkono vizuri sana na wenzetu wametuwakilisha vizuri kabisa. Lililobaki sasa ni kuwahoji kilichopo mbele yetu, kinachohitaji uamuzi wenu ni kupitisha Azimio la kumpongeza mtu wa kwanza mwenye asili ya Afrika kuchaguliwa kuwa Rais wa Marekani (*USA*), ambaye ni Barack Obama.

Waheshimiwa Wabunge sasa tuiamue hoja iliyopo mbele yetu.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Azimio la Kumpongeza Rais Mteule wa Marekani
liliridhiwa na Bunge)*

SPIKA: Kwa hiyo, nafurahi kutangaza kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo tarehe 05 Novemba, 2008 limepitisha rasmi, Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Barack Obama, kwa ushindi wake mkubwa wa kuwa Rais wa kwanza wa asili ya Kiafrika kutawala nchi ya Amerika. Kwa hiyo, nitalifikisha rasmi Azimio hili katika mikondo ya Serikali ili liweze kuwafikia kule Washington DC.

Waheshimiwa Wabunge, kwa shughuli ambazo zilipangwa siku ya leo ndio tumefikia mwisho na kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho tarehe 06 Novemba, 2008 saa tatu asubuhi.

*(Saa 05.40 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 06 Novemba, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*